# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 14 | Desemba 4, 2022 JARIDA LA JUMAPILI BILA MALIPO




# MAOVU YA RIADHA ZA KENYA

**Tunakuletea habari za ndani kuhusu janga la pufya, ambapo maajenti matapeli wanashirikiana na wanariadha kudanganya. Vitendo vyao vinatishia kuchafua sifa za nchi kama bingwa wa riadha duniani**

# *The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore*

# anywhere, anytime.


Follow the link to subscribe

> *epaper.nation.africa.*

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play




Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111

Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

## Yaliyomo

**9 UTAWALA USIO NA MPANGO:** Mgongano wa majukumu kati ya Waziri wa Kilimo Mithika Linturi na mwenzake wa Biashara, Moses Kuria unaweza kuwa ishara za mapema za mivutano katika serikali ya Rais William Ruto.

**13 FUNDI WA RAIS:** Ashok Sunny anashona suti za kifahari kwa kutumia vitambaa vya ubora wa hali ya juu na kushonwa kwa mikono, na ingawa nguo zake zinaweza kuonekana ghali, hakosi wateja.



**22** Kutoka Olimpiki hadi Kombe la Dunia la Fifa, wanariadha wameonyesha uwezo wao wa kuwa msitari wa mbele katika vita dhidi ya ubaguzi wa rangi.

**25 VITA VIKALI DHIDI YA AL-SHABAAB:** Serikali ya Somalia imekumbatia mbinu kadhaa katika vita dhidi ya kundi hili mwanachama wa Al-Qaeda ambalo, licha ya ufanisi wa mapema wa kijeshi, inaoenekana kuwa ndefu na ngumu.

*- Zimetafsiriwa na Benson Matheka*

# Namwamba aache kumbukumbu kwa kusafisha riadha nchini Kenya

Kenya bila wanariadha wake maarufu haivutii, ni sawa na chai isiyo na majani chai. Kwa miongo sita, Kenya imeacha alama katika ulimwengu kama nchi maarufu kwa riadha. Watu wengi kote duniani wanasikia nchi inayoitwa Kenya kupitia ushindi wa wana na binti zake katika riadha.

Uvumishaji bila malipo ambao wanariadha wetu wametupatia ungegharimu Wizara ya Fedha mabilioni ya dola kununua nafasi ya kujitangaza. Hata hivyo, mambo sio shwari katika masuala ya riadha.

Wanariadha zaidi ya 30 wa Kenya, wengi wao maarufu, wamepigwa marufuku katika mwaka mmoja uliopita kwa kikiuka sheria za kutumia dawa za kusisimua misuli. Asilimia 40 ya visa vyote vilivyothibitishwa vya pufya mwaka huu vinatoka Kenya.

Uadilifu wa utendaji wa wanariadha wetu umetiliwa shaka, na Shirika la Kukabiliana na Pufya Ulimwenguni linatupiga darubini kwa karibu. Ongezeko la visa hivi vya pufya limefanya Kenya kuorodheshwa katika 'Kundi A', la nchi ambazo pufya inatumika kwa wingi. Ni nchi zingine tatu ambazo ziko katika orodha hii;Ethiopia, Belarus and Ukraine.

Historia ya ushindi ambao wanariadha wetu wamepata kwa miaka mingi inatishiwa kuharibiwa na ulafi wa wanariadha wachache, maajenti na mameneja wao.

Makala ya kina katika toleo la wiki hii yanaangazia ulimwengu wa giza wa pufya na kufichua desturi ambayo inafanana na mafia inayoibuka ya wanaoendeleza na kunufaika na ulimwengu huu wa giza. Hakika ni hadithi ya kutisha inayoelezea uharibifu wa kujisababishia katika sekta ambayo ina pesa nyingi.



**Washington Gikunju**

**Ni rahisi kurudia hali hiyo kwa kuwa sasa hakuna tishio la marufuku na kuzama zaidi katika shimo la kina kirefu, kwa kuzingatia tajiriba ya siku zilizopita. Juhudi za Waziri Namwamba ambazo zilileta afueni dakika ya mwisho kwa wanariadha waaminifu na wenye bidii haifai kuwa ya kuahirisha tatizo, kama ilivyofanyika wazi miaka sita iliyopita**

Ahadi ya serikali ya kuongeza ufadhili kwa vita dhidi ya pufya, kwa kuzitengea Sh619 milioni kila mwaka kwa miaka mitano ijayo, ilisaidia kuepuka marufuku kutoka mashindano ya ulimwengu mwezi uliopita.

Marufuku kama hiyo ingezamisha ndoto za wanariadha wengi wenye matumaini, wasiweze kuyafufua tena, ikizingatiwa kuwa mtu hawezi kushiriki riadha kwa miaka mingi.

Waziri wa Michezo, Ababu Namwamba, aliokoa nchi baada ya kuandika barua kwa Shirikisho la Kimataifa la Riadha akieleza mpango wa kuimarisha uhamasishaji, kutekeleza hatua za kupiga vita pufya na kuongeza ufanyaji wa vipimo.

Ni lazima hii izindue wanaohusika na michezo nchini. Ni rahisi kurudia hali hiyo kwa kuwa sasa hakuna tishio la marufuku na kuzama zaidi katika shimo la kina kirefu, kwa kuzingatia tajiriba ya siku zilizopita.

Kenya ilinusurika kufuata njia ya Urusi na iliruhusiwa kushindana katika Michezo ya Olimpiki ya Rio mnamo 2016 baada ya Rais Uhuru Kenyatta kutia saini Sheria ya kupiga vita Pufya, ambayo ilianzisha shirika la kukabili pufya na mfumo wa sheria.

Hatua ya Waziri Namwamba ambayo ilileta afueni dakika ya mwisho kwa wanariadha waaminifu haifai kuwa ya kuahirisha tatizo, kama ilivyofanyika wazi miaka sita iliyopita. Juhudi za kuinua michezo safi lazima zianzishwe mara moja, kudumishwa na kuendelezwa.

Ujumbe wa kuangamiza pufya unafaa kuwa kauli mbiu katika hafla na majukwaa yote ya wanariadha, wakufunzi na washikadau wengine. Maajenti wanaowania utajiri wa haraka, wakufunzi, maajenti, mameneja na maafisa waliopotoka lazima wapigwe marufuku kabisa. Iwapo Waziri Namwamba anaweza kufanya hili kuwa mradi wake wa kukumbukwa wa mapema katika muhula wake, unatosha kumpatia nafasi katika vitabu vya historia.

***wgikunju@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Darubini ya Wiki
Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno
**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Joe Ageyo** Mkurugenzi wa Uhariri
**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji
**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

■ 'Opaque 4' mashakani kuhusu uchaguzi

# Azimio kuandaa mikutano

Viongozi wa Muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya mnamo Desemba 7 wataanza mikutano kote nchini na maandamano kulalamikia mipango ya kutimua makamishna wanne wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC). Mikutano hiyo na maandamano dhidi ya serikali ilipangiwa kuanza Novemba 30, lakini kiongozi wa Azimio Raila Odinga akatangaza kuwa iliahirishwa ili kutoa nafasi kwa mitihani ya kitaifa kuendelea bila kutatizika.


Walilaumu serikali ya Kenya Kwanza kwa kuwaandama makamishna hao wanne kwa kukataa matokeo ya uchaguzi wa urais wa Agosti 9.

Pia walitaja uamuzi wa kuagiza mahindi ya GMO, ukosefu wa usalama na gharama ya juu ya maisha kuwa baadhi ya sababu za mikutano hiyo.

Wakati huo huo, Bunge la Kitaifa linatarajiwa kuandaa kikao maalumu cha kujadili ripoti ya Kamati ya Haki na Masuala ya Sheria kuhusu tabia ya makamishna hao wanne.


Kamati hiyo imekuwa ikishughulikia maombi manne yaliyowasilishwa dhidi ya Cherera na wenzake wanne kwa wiki mbili zilizopita, kusikiliza walalamishi na mawakili wa makamishna hao.

Mnamo Alhamisi wiki jana, kamati iliwasilisha ripoti mbele ya Bunge la Kitaifa.



Viongozi wa Azimio la Umoja-One Kenya Kalonzo Musyoka, Raila Odinga na Martha Karua.

■ Itakuwa hatua ya kwanza ya muafaka, anasema



Tiger Woods akicheza wakati wa shindano la Masters katika Augusta National Golf Club mnamo Novemba 12, 2020.

# Woods: Greg Norman 'lazima aondoke'

Tiger Woods anasema Greg Norman "lazima aondoke" kama kamishna wa shindano la LIV Golf Series kama msururu ujao utaendelea kwa Amani kati ya US PGA na DP World.

Akizungumza Jumanne katika shindano lake la Hero World Challenge katika Albany, Bahamas Bingwa mara tano wa shindano kuu alisisitiza kauli zilizotolewa mapema mwezi huu na nyota wa Northern Ireland, Rory McIlroy, wote wawili wakisema kesi kati ya pande zote mbili zinafaa kuondolewa iwapo hatua zitapigwa. "Kuna fursa hapo nje iwapo mashirika yote mawili yatasimamisha kesi zake," akasema Woods.

"Hiyo ndio shida. "Huwezi kuwa na nia nzuri ya kujadiliana kama kuna kesi dhidi yako. Nafikiri ni lazima Greg aondoke kwanza. Ni lazima ianze na uongozi upande wao, kuelewa kuwa kinachofanyika sasa hivi sio kitu kizuri kwa hali ya baadaye ya gofu. Unahitaji kuleta pamoja pande zote na kama kuna upande ulio na chuki nyingi kiasi cha kujaribu kuharibu shindano letu, basi unaweza kufanya nini la hilo?"

Norman amekuwa sura ya makabiliano ya upande uliojitenga ambao unafadhiliwa na Hazina ya Uwekezaji wa Umma ya Saudi Arabia. Mnamo Septemba alisema hakuwa na nia ya kuzungumza na upande mwingine katika juhudi za kumaliza mgawanyiko uliosababishwa na LIV Golf kurai baadhi ya majina makubwa kwa pesa nyingi kwa mashindano ya mashimo 57.

■ Alimlaumiwa kwa kuruhusu ufisadi

# Memes China wakiomboleza Jiang



Wakitumia memes za marehemu "toad king" na kumbukumbu za enzi iliyoonekana kuwa yenye uhuru zaidi - raia wa China waliingia katika mitandao ya kijamii Jumatano kuomboleza kifo cha aliyekuwa kiongozi Jiang Zemin. Zaidi ya maoni milioni moja yalitolewa ndani ya saa moja baada ya ujumbe wa runinga ya serikali CCTV wa kutangaza kifo chake, huku wengi wakimuita "Babu Jiang". Kuna mseto wa hisia kuhusu Jiang - wengi walikaribisha ucheshi wake katika umma kama pumzi mpya baada ya miongo mingi ya uongozi wa kikomunisti huku wakosoaji wakimlaumu kwa kuruhusu ufisadi.

■ Operesheni Desert Light: Usambazaji wazimwa

# Europol yazima 'mtandao' wa kokeni




Mtandao mkubwa unaodhibiti thuluthi moja ya uuzaji wa kokeni Ulaya umevunjwa, polisi wametangaza. Katika msako kwa jina Operesheni Desert Light, watu 49 walikamatwa katika nchi sita za Ulaya, Shirika la polisi la Muungano wa Ulaya, Europol, lilisema. Walijumuisha raia wa Uingereza, anayeshukiwa kuongoza biashara hiyo. Zaidi ya tani 30 (kilo 30,000) za dawa zilikamatwa, Europol ilisema. Serikali za Uhispania, Ufaransa, Ubelgiji, na Uholanzi na Milki ya Kiarabu zilishirikiana kuvunja mtandao huo. Miongoni mwa waliokamatwa ni watu sita waliolengwa – ambao walikuwa wakisakwa na polisi wa kimataifa.

*- Zimetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ MAAJENTI WANAOTAFUTA UTAJIRI WA HARAKA KWA VYOVYOTE VILE

# JANGA LA PUFYA: UKWELI

## Kenya – nchi maarufu kwa riadha - imeorodheshwa chini ya 'Kundi A' na Wada, kumaanisha nchi iliyo na kiwango kikubwa cha udanganyifu




• NA OMULO OKOTH

Ni ajabu kuwa Kenya haijabanduliwa kutoka riadha ulimwenguni. Wengi wa wanariadha wake wamehusishwa na usisimuaji misuli hivi kwamba nchi, ambayo kwa miongo mingi imejulikana kwa ubingwa wa mbio za kati na ndefu, ina bahati kutopigwa marufuku na Shirika la Kukabiliana na Pufya Ulimwenguni (Wada).

Ushindi wa wanariadha wa Kenya katika mbio za marathon katika miji mikubwa, kusema kweli, ulipokewa kwa shaka na kibaya zaidi, dharau. Hata hivyo, wengi wao bado wanatia bidii kushiriki riadha, kufuatia nyayo za watangulizi wao kama Nyantika Maiyoro, Kanuti Sum, Kipchoge Keino, Wilson KIprugut Chumo, Ben Jipcho, Daniel Rudisha, Charles Asati, Robert Ouko, Sabina Chebichi, Rose Tata Muya, Tecla Chemabwai na mamia ya wengine ambao waliamini katika kutia bidii.

Janga la utitimuaji misuli limebadilisha kabisa riadha ulimwenguni, kwa sababu ya maajenti wanaotaka kupata utajiri wa haraka, ambao wanahusisha wakufunzi, mameneja na maafisa waliopotoka na ambao wako tayari tu kunufaika, bila kujali matokeo yake.

Kwao, haijalishi mbinu wanayotumia kufaidika. Wanariadha wachanga wasio na habari wamekuwa wakitumiwa vibaya na mara nyingi kuongozwa kutumia vinywaji, tembe au kudungwa sindano zilizo na dawa za kusisimua misuli ambazo athari zake kwa mwili zinaweza kusababisha kifo.

Wakati mwingine, huwa wanashirikishwa katika ukandaji wa misuli na mchakato spesheli wa kisayansi ambao unakuwa wa

Endelea Uk 6

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

# Sababu za wanariadha Kenya kutumia dawa

Kutoka Uk 5

kuweka damu iliyo na oksijeni, mchakato unaofahamika kama pufya ya damu.

Ingawa hii inasaidia wanariadha kushinda mbio, na pesa nyingi, athari zake kwa mili yao haiwezi kulinganishwa na thamani ya dola wanazopokea. Baadhi yao wamezirai na kufa katika hali zisizoeleweka, huku wengine wakiharibiwa kabisa afya yao ya uzazi.

Maafisa wa riadha, ambao wanapaswa kuwa wakiongoza vita vya kulinda wanariadha, hawajajitokeza kuchukua msimamo wa wazi kuhusu suala hili. Baadhi yao nchini Kenya wamelaumiwa kwa kulinda maajenti wanaohusika na kuendeleza vitendo vya kusisimua misuli wanariadha.

Ni kwa sababu hii ambapo serikali iliunda Shirika la Kukabiliana na Pufya la Kenya (ADAK) kupitia Sheria ya Bunge kusaidia kusukuma ajenda ya kupiga vita janga hilo.

Lakini bila nguvu na kutokuwa na jukumu la kutoa adhabu ambayo kuzuia wanariadha kutumia dawa, jukumu la ADAK limebaki kuwa kuhamasisha wanariadha kuhusu hatari za kutumia dawa za kusisimua misuli.

Lakini haliwezi kuwasimamisha au kuwapiga marufuku kushindana, ikizingatiwa kwamba pia linatumia sheria za Wada ambazo Kenya imekumbatia.

ADAK hutumia mamilioni ya pesa za mlipa ushuru kila mwaka wa kifedha kutuma maafisa wake kote nchini, lakini kila mwezi, wanariadha wa Kenya wanapatikana wamekiuka sheria za kukabiliana na usisimuaji wa misuli.

Kuna fisi wengi katika uwanja wa michezo kwa jumla, hasa katika riadha, wanaojifanya kujali wanariadha lakini wanashirikiana na mameneja wakora kuendeleza uovu huo.

Tofauti na Urusi, na iliyokuwa nchi ya kikomunisti ya Ujerumani Mashariki, zinazoendesha mipango ya usisimuaji misuli, serikali ya Kenya haijawahi kuhusika na uongezaji nguvu wanariadha wake kisayansi. Hii ndiyo imefanya nchi kutopigwa marufuku kushiriki mashindano ya kimataifa, ingawa imeorodheshwa miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa usisimuaji wa misuli.

Chama cha Riadha Kenya, kama shirika muhimu, hakijawahi kuunga mkono usisimuaji wa misuli pia, lakini kina baadhi ya maafisa wake, wa zamani na wanaohudumu, ambao wamekuwa wakishirikiana na wataalamu wa usisimuaji misuli kuendeleza uovu huo miongoni mwa wanariadha wa Kenya. Baadhi ya maafisa wanafanyia kazi mameneja au maajenti, baadhi ambao ni hatari kama manyapara wa watumwa.

Ajenti mmoja aliwahi kuniambia kuwa asilimia 95 ya wanariadha maarufu huwa wanatumia dawa za kusisimua misuli, na kwamba maafisa kutoka mashirikisho ya kimataifa hadi matawi yake huwa wanahusika au wanajua kinachoendelea.

Haikuchukua muda mrefu ukweli kuibuka baada ya shirikisho zima la kimataifa na washirika wake kuporomoka huku kukiwa na madai ya njama za hongo na kufichwa kwa ufichuzi kuhusu usisimuaji misuli kwa kiwango kikubwa.

Mtu akikamatwa, hakuna anayekuwa tayari kuwajibika. Wanariadha wanaachwa kubeba msalaba wao. Maajenti wanajitenga nao na ghafla wanawajibika kwa kilichoingia katika mili yao. Hata wanariadha wenzao wanawakana.




Rita Jeptoo akisherehekea ushindi katika mbio za Marathon za Chicago mnamo Oktoba 12, 2014. PICHA I MAKTABA

Aliyekuwa mshindi wa mbio za Boston na Chicago, Rita Jeptoo, alipofeli kipimo cha usisimuaji misuli mnamo 2016, waliokuwa katika kundi lake la usimamizi waliitisha kikao cha wanahabari kujitenga naye.

Jeptoo alikuwa mmoja wa wanariadha maarufu kuwa waathiriwa wa janga la usisimuaji misuli katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Wengine ni aliyekuwa bingwa wa ulimwengu na Olimpiki Asbel Kiprop na bingwa wa mbio za Rio mwaka wa 2016, Jemimah Sumgong.

Baadhi yao wameondolewa kesi baada ya

**Wanaotaka kusisimua misuli watajuta. Tunataka kushirikiana na Kitengo cha Maadili cha Wanariadha (AIU). Wanaotaka kudanganya wahesabu siku zao; hakuna njia ya mkato kufaulu. Tumejitolea kulinda wanariadha walio safi; hatutakuwa na huruma na wachache wanaodanganya ambao wanataka kutuingiza katika kitu hiki.**

Chama cha Riadha Kenya

Nation Media Group "ePaper Copy"

marufuku, lakini huwa ni ushindi ghali sana baada ya kulipa ada za juu za kisheria na majina yao kupakwa tope.

Wanahabari wanaothubutu kufichua uovu huu kwa kuhimiza adhabu kali na kupigwa marufuku kwa maajenti wa wanariadha wanaodanganya husemwa vibaya na wenzao, huku wenzao wanaofanya wanavyotakiwa kufanya wakikumbatiwa kama 'familia' na kuteuliwa kwa nyadhifa za ushauri.

Maafisa wa chama cha wanariadha Kenya wanajua ni nani miongoni mwao anahusiana na kampuni za usimamizi ambazo wanariadha wake wamenaswa katika ulimbo wa usisimuaji wa misuli. Maafisa wa kiufundi wanaoshukiwa kushirikiana na wanaoendesha usisimuaji misuli wanapoteuliwa kwa timu za taifa, au kwa kamati zinazosemekana kuwa za kupiga vita uovu huo, je wanaowateua wanatarajia watu waseme nini?

Maafisa wengi, wakijumuisha wanahabari wanaopaswa kufichua maovu kama hayo hunufaika na sherehe au safari kutoka kwa wanaohusika na usisimuaji misuli. Hii ndiyo sababu ilikuwa ni lazima vita dhidi ya usisimuaji misuli kufeli na kufeli vibaya.

Usisimuaji misuli unahusisha mitandao, kuanzia kiwango cha kimataifa na kushuka hadi mashirikisho wanachama, maafisa muhimu, kampuni za dawa, idara za usalama, wanahabari na madaktari. Juhudi zozote kutoka kwa mtu aliye na nia njema, hasa mwanahabari, za kuanika njama hizi zinazua uhasama, kutengwa na kukosa kualikwa kwa hafla za kimataifa.

Miaka minne iliyopita, maabara iliyoidhinishwa na Wada ilianzishwa Nairobi kupima sampuli za damu. Ulimwengu wa spoti uliambiwa hii ingefanya upimaji kuwa nafuu. "Kila kitu kitakuwa rahisi, maabara hii itasaidia kupigana na uovu huu, na hatutakuwa tukienda nje ya nchi. Itakuwa hapa karibu, mambo yatakuwa haraka, rahisi na nafuu," tuliambiwa.

"Wanaotaka kushiriki usisimuaji misuli watajuta. Tunataka kushirikiana na Kitengo cha Maadili cha Wanariadha (AIU). Wanaotaka kudanganya wahesabu siku zao; hakuna njia ya mkato kupata ushindi. Tumejitolea kulinda wanariadha walio safi; hatutakuwa na huruma na wachache wanaodanganya ambao wanataka kutuingiza katika kitu hiki," wakasema maafisa wa AK.

AK ilianzisha Mtandao wa Madaktari Kenya, ambao, hatua ambayo maafisa wake walisema, ilisaidia katika vita dhidi ya usisimuaji misuli. AK pia ilianzisha Kamati ya Idara tofauti ya Kukabiliana na Usisimuaji wa Misuli kwa ushauri wa AIU. Lakini usisimuaji misuli uliendelea tu.

Kati ya 2004 na Agosti 1, 2018, jumla ya wanariadha 138 kutoka Kenya (kutoka michezo yote) waligunduliwa kuwa walitumia dawa zilizopigwa marufuku.

Miongoni mwao (ni 131 walionaswa wakishiriki mashindano au wasiokuwa kwenye mashindano).

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*



## Baadhi ya wanariadha wa Kenya waliokiuka sheria za utumiaji dawa za kusisimua misuli mwaka huu

1. Ibrahim Makunga Wachira
2. Kenneth Kiprop Renju
3. Michael Kanyunga Njenga
4. Johnstone Kibet Maiyo
5. Lawrence Cherono
6. Mark Kangogo
7. Philemon Kacheran
8. Felix Kipchumba Korir
9. Emmanuel Saina
10. Joel Maina Mwangi
11. Matthew Kisorio
12. Justus Kimutai
13. Morris Munene Gachaga
14. Edward Kibet Kiprop
15. Paul KIpchumba Lonyangata
16. Kumari Taki
17. Marius Kipserem
18. Diana Chemtai Kipyokei
19. Eglay Nalianya
20. Lilian Kasait
21. Stella Barsosio
22. Purity Changwony
23. Betty Wilson Lempus
24. Vane Nyaboke
25. Tabitha Gichia Wambui
26. Joyce Chepkirui
27. Purity Jerono Talam
28. Teddy Otengo
29. Everylne Syombua
30. Phenus Kipleting
31. Gloria Kite
32. Daniel Wanjiru

Aliyekuwa Bingwa wa Dunia mara tatu katika mbio za mita 1,500, Asbel Kiprop, akifanya mazoezi katika Uwanja wa Michezo wa Kipchoge Keino mjini Eldoret mnamo Februari 4 baada ya marufuku ya miaka minne kwa kutumia dawa. PICHA |JARED NYATAYA

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

NJAMA ZA KISIASA ZA KUMFUNGIA RAILA NJE

# SIKIO LA MUDAVADI MASHINANI

**Malalamishi ndani ya ODM kuhusu ugavi wa nafasi za uongozi bungeni yanampa Mkuu wa Mawaziri nafasi ya kunasa wabunge wa Magharibi**

Na OSCAR OBONYO

Ukifanywa wakati ambao Naibu Rais Rigathi Gachagua anaendelea kujijenga kisiasa katika eneo la Mlima Kenya huku aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga akiwa katika baridi ya kisiasa baada ya kushindwa katika uchaguzi mkuu wa Agosti 9, mkutano wa Mkuu wa Mawaziri Musalia Mudavadi na wabunge wa Magharibi mwa Kenya uliwadia wakati unaofaa na ulikuwa na uzito.

Gachagua na Odinga huenda wakawa kizingiti kwa Mudavadi kufikia ndoto yake ya muda mrefu ya kuwa urais. Si ajabu basi kuwa mkutano huo wa Novemba 22 ulichukuliwa kuwa wenye umuhimu mkubwa wa kisiasa kudhibiti malengo na nia ya Naibu Rais na kufaidi kutokana na makosa ya Odinga katika ulingo wa siasa.

Kwa miaka mingi, kiongozi huyo wa ODM amelaumiwa kwa kusaliti uamunifu wa wafuasi wake kutoka Magharibi mwa Kenya kwa madai ya kutowagawia nafasi anazopata kila baada ya uchaguzi.

Kilichokasirisha wanasiasa kutoka eneo hilo, hasa wanaotoka Kaunti ya Kakamega, ni kuwa, ingawa kaunti hiyo ilimpa Odinga kura nyingi katika uchaguzi mkuu wa Agosti, ODM haikumpa mbunge yoyote kutoka eneo hilo wadhifa mkuu wa uongozi wa kamati za bunge. Miongoni mwa wabunge 12 kutoka Kakamega, tisa walichaguliwa kwa tiketi ya ODM, wawili kupitia ANC na mmoja kwa tiketi ya Development Action Party of Kenya (DAP-K).

Gavana Fernandes Barasa na Mbunge Mwakilishi wa Kike Elsie Muhanda nao walichaguliwa kwa tiketi ya ODM. Chama hicho pia kilivuna kura nyingi zaidi katika kaunti za Busia na Vihiga.

Kwa nini baada ya kuungwa mkono kiasi hicho na watu wa Magharibi, ODM haikupatia eneo hilo nafasi stahiki za uongozi bungeni?

Mbunge wa Navakholo, ambaye alihudumu kama Kiranja wa Wengi katika Bunge la 12, hakuteuliwa katika wadhifa wowote wa uongozi wa bunge au kamati zake. Opiyo Wandayi na Junet Mohamed, wote wawili kutoka Luo Nyanza, waliteuliwa Kiongozi wa Wachache na Kiranja wa Wachache, mtawalia.


Uhasama kati ya wabunge wa Magharibi mwa Kenya na wenzao wa Nyanza unaendelezwa zaidi na maelewano kabla ya uchaguzi mkuu ambapo Mbunge wa Westlands, Tim Wanyonyi, alishawishiwa kujiondoa katika kugombea Ugavana wa Nairobi na kumpa nafasi Polycarp Igathe wa Jubilee. Wakati huo, iliaminika Wanyonyi angeshinda kiti hicho.

Katibu Mkuu wa ODM, Edwin Sifuna, pia amevunjwa moyo baada ya kuondolewa kwenye wadhifa wa uongozi katika Seneti. Alikuwa ameteuliwa Naibu Kiranja wa Wachache lakini baadaye wadhifa huo ukapewa Seneta wa Narok, Ledama Ole Kina.

Hakuna mbunge kutoka jamii ya Waluhya anashikilia nafasi yoyote kati ya nne za juu za uongozi katika bunge. Ukweli huu ndio chanzo cha hasira kutoka kwa wabunge wa Magharibi mwa Kenya ambazo Mudavadi anaweza kutumia kwa manufaa yake kisiasa.

Huenda hii ndiyo maana alialika wabunge kutoka Magharibi mwa Kenya kwa mkutano wa jijini Nairobi. Katika ujumbe kupitia mtandao wa kijamii, Mudavadi alisema walijadili na kukubaliana kwa pamoja.

"Nilifanya majadiliano mazuri na yenye faida na wabunge kutoka Magharibi mwa Kenya. TuliKUbaliana na viongozi na kupalilia umoja, ugavi wa rasilimali za kitaifa kwa maendeleo ya eneo letu. Ustawi wa nchi yetu utaendelezwa kama viongozi wataungana na kuendeleza masilahi ya watu," akasema Mkuu wa Mawaziri baada ya mkutano huo.



Ikumbukwe kuwa mkutano wa Mudavadi ulifanywa siku moja baada ya Naibu Kiongozi wa ODM Wycliffe Oparanya kuripotiwa kutangaza kuwa amevunja uhusiano wake na Odinga na sasa ataelekeza juhudi na nguvu zake katika kuunganisha jamii ya Waluhya.

Baadaye Oparanya alikana madai ya kutoa matamshi hayo. Lakini Wandayi anasema hii ni nchi inayoheshimu demokrasia na haki ya kutangamana inafaa kufurahiwa na kila raia. Wandayi, ambaye pia ni Katibu wa Masuala ya Kisiasa katika ODM, anatoa sababu kuwa muungano wa Azimio haukuunda serikali. "Hatuko mamlakani, hivyo nafasi zilizopo za kugawanywa bungeni ni chache zaidi. Sio rahisi kuridhisha kila mtu," anasema.

Tangu kuondolewa kwake kama Mbunge wa Sabatia 2002 na Moses Akaranga, Mudavadi hajawahi kudhibiti eneo la Magharibi. Miongoni mwa sababu zilizochangia hali hiyo ni kujiondoa kwake katika kinyang'anyiro cha urais mwaka huo kukwepa kupambana na wagombeaji nyota. Badala yake aliunga azma ya urais ya Uhuru Kenyatta, mwanasiasa chipukizi, aliyekuwa amehudumu kwa mwaka mmoja kama mbunge mteule.

Nyota ya Mudavadi katika siasa iling'aa tena miaka mitano baadaye, aliposhirikiana na Odinga na William Ruto katika ODM. Alipanda ngazi hadi akahudumu kama Naibu Waziri Mkuu katika Serikali ya Muungano Mkuu kufuatia ghasia za baada ya uchaguzi mkuu wa 2007; ambapo Odinga na Mwai Kibaki walikabiliana katika kinyang'anyiro cha urais.

Alipogombea urais 2013 kwa tiketi ya chama cha United Democratic Forum (UDF), Mudavadi alipata maseneta wawili na wabunge 11. Lakini baadaye udhibiti wake wa eneo la Magharibi ulilegea kiasi kwamba wakati huu chama chake, ANC kina wabunge saba pekee, kikilinganishwa na wabunge 16 (13 katika bunge la kitaifa na watatu katika Seneti) katika Bunge la 12.

Akionekana kulenga kusambaza ushawishi wake nje ya Magharibi mwa Kenya, Mudavadi amejiuzulu kama kiongozi wa ANC na kumkabidhi wadhifa huo Gavana wa Lamu, Issa Timamy. Hii ni baada ya kuteuliwa kwake kuwa Mkuu wa Mawaziri. Mbunge wa Matuga (ANC) Kassim Tandaza anasema hatua hiyo itaimarisha ANC eneo la Pwani.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ HALI YA KUCHANGANYIKIWA SERIKALINI

# NI UTAWALA USIO NA MPANGO

## Mgongano wa kimajukumu kati ya Linturi (Kilimo) na Kuria (Biashara) huenda ukawa dalili za mapema za mivutano katika serikali ya Ruto

● NA JOHN KAMAU


Moses Kuria


Mithika Linturi

Kinachoonekana kuwa mgongano wa kimamlaka kuhusu uagizaji wa mahindi, huenda kikawa mivutano mikali kati ya Waziri wa Biashara Moses Kuria na mwenzake wa Kilimo, Mithika Linturi. Inaweza pia kuwa dalili ya migawanyiko katika Baraza la Mawaziri la Rais William Ruto kuhusu majukumu yao.

Hii si mara ya kwanza hali hii imeshuhudiwa. Majuzi, Naibu Rais Rigathi Gachagua alitangaza akiwa Nyeri kuwa alishinikiza wabunge wa Mlima Kenya kumchagua mtu kutoka upinzani, Kanini Kega, kujiunga na Bunge la Afrika Mashariki (EALA).

Hatua hiyo ilikinzana na matakwa ya Rais Ruto, aliyekuwa ameidhinisha orodha tofauti. Hilo, na mikwaruzano ya kimamlaka kati ya Linturi na Kuria, linaweza kuwa dalili za mapema kuhusu mivutano inayoendelea katika serikali ya Rais Ruto.

Kiangazi kilipoendelea kukumba nchi, Kuria ndiye amekuwa akitangaza mipango ya kuagiza mahindi na pia alikuwa wa kwanza kutangaza kuwa nchi itaagiza vyakula vilivyokuzwa kisayansi. Siku chache baadaye, Linturi - aliyekuwa amebaki kimya - alisema "hajui chochote" kuhusu mipango hiyo.

Kuria alisema serikali ilipanga kuagiza mahindi hayo kujaza akiba katika maghala ya kitaifa – ambalo ni jukumu Wizara ya Kilimo. Haijabainika ni kwa nini Kuria aliingilia kazi ya Wizara Kilimo.

Ukitazama historia kuhusu mkanganyiko kama huu, unaanza kuelewa jinsi ya kufasiri migongano kama hiyo. Kihistoria, migongano kama hiyo katika biashara na siasa ilikuwa makusudi. Inaweza kuwa pia imepangwa.

Katika miaka ya 1960, Tom Mboya alikuwa akikiuka majukumu ya wizara yake kuleta hoja za serikali bungeni, kwa kumpita Makamu wa Rais na Kiongozi wa Shughuli za Serikali, Oginga Odinga. Ikizingatiwa kuwa wabunge hawakufahamu iwapo hoja za Mboya zilikuwa za serikali ama zake binafsi, angezitumia kumkasirisha Jaramogi - kwa niaba ya watu na taasisi nyingine zilizomtaka kuondolewa.

Kisa kingine kilitokea 1963 wakati Wizara ya Elimu, wakati huo ikiwa chini ya Joseph Otiende, ilipokea nafasi za ufadhili wa masomo kutoka Bulgaria. Baada ya kubaini Wakenya ambao wangefaidika kutokana na nafasi hizo, na dakika chache kabla yao kupanda ndege, Mboya na Dkt Njoroge Mungai walibadilisha wanafunzi wa Otiende na badala yake wakatoa nafasi hizo kwa vijana 55 wafuasi sugu wa Kanu. Hilo lilifanywa katika uwanja wa ndege, hali iliyomkasirisha sana Bw Otiende, aliyeuliza: "Tuna serikali ngapi katika nchi hii?"

Moja ya sababu za kutofaulu kwa mradi wa kilimo cha ekari milioni moja nchini miaka ya 1960 ilikuwa ni mvutano baina ya Waziri wa Kilimo Bruce Mackenzie na mwenzake wa Ardhi na Makao, Jackson Angaine. Hilo pia lilimhusisha Waziri wa Fedha James Gichuru. Wakati mmoja, akishughulikia suala la maskwota, Gichuru alituma barua ya siri kwa Angaine iliyoandikwa Februari 14, 1966, akimkumbusha: "Kama unavyojua," ikaeleza barua hiyo, "sera ya serikali ni kutompa mtu wa hadhi yoyote ile nchini ardhi bila malipo."

Angaine hakufurahia: "Sikumbuki popote niliposema maskwota wapewe ardhi bila malipo au kuwa pesa zinazotumika kuwapa makao hazipaswi kurudishwa," akamjibu. Angaine alishikilia kuwa Gichuru hakuwa akipewa ushauri unaofaa na maafisa wake. "Kutokana na haya, sioni haja ya kuendelea kufanya mikutano zaidi ila tu iwe katika kiwango cha uwaziri," akaandika na kutuma nakala za barua hizo kwa Mwanasheria Mkuu Charles Njonjo, McKenzie na Mboya.

Wakati wa utawala wa Rais Moi, kulikuwa na mizozo ya mapema kati ya Njonjo na Waziri wa Fedha Mwai Kibaki, katika kinachoelewekа sasa kuwa mizozo ya ubabe. Ingawa Moi aliwadhibiti vizuri mawaziri wake – ilikuwa nadra kwao kukosoana, kujiuzulu kwa Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano Kenneth Matiba kulikosolewa waziri mwingine.

Hata hivyo, ni wakati wa utawala wa Kibaki ambapo mawaziri walilaumiana sana. Mivutano iliyobainika sana ilikuwa kati ya Kibaki na Waziri Mkuu, Raila Odinga, kutokana na ufasiri wa majukumu waliyogawana.

Wakati mmoja, Waziri Mkuu alimwachisha kazi kwa muda William Ruto, wakati huo akiwa Waziri wa Kilimo, kutokana na sakata ya mahindi – lakini akarudishwa kazini na Rais Kibaki. Ni wakati huo pia ambapo Waziri wa Haki na Masuala ya Kikatiba Martha Karua alijiuzulu Aprili 6, 2009, baada ya kutofahamishwa na Rais Kibaki na Mwanasheria Mkuu kuhusu uteuzi wa majaji.

Makabiliano mengine yalitokea kati ya Wizara ya Ustawi wa Kikanda ya Fred Gumo, na ya Kawi, ya Kiraitu Murungi, kuhusu udhibiti wa mradi wa kuzalisha kawi ya upepo katika Wilaya ya Marsabiti Kaskazini. Wote walikuwa wakipigania kuwa na usemi katika mradi huo tata wa mabilioni ya pesa.

Mnamo Oktoba 2008, Waziri wa Huduma za Afya Anyang' Nyong'o alitangaza kuwa Kenya ilikuwa imeondolewa katika Hazina ya Dunia kwa kukosa kueleza jinsi ilivyotumia mabilioni ya pesa ilizopewa. Lakini mwenzake wa Afya ya Umma, Beth Mugo, alitoa kauli tofauti, akisema hakukuwa na hatua kama hiyo.

Sasa katika utawala wa Rais Ruto, Mawaziri wanaonekana kutoa kauli zisizohusu wizara zao - au bila kutafuta ushauri. Kwa mfano, Waziri wa Elimu Ezekiel Machogu alilazimika kubadilisha msimamo wake baada ya kutoa kauli kuhusu elimu ya vyuo vikuu. Baadaye, alilaumu vyombo vya habari.

Waziri wa Utumishi wa Umma, Aisha Jumwa, majuzi aliondoa marufuku kuhusu 'disko matanga' Kilifi, iliyokuwa imewekwa na aliyekuwa Waziri wa Usalama wa Ndani Fred Matiang'i.

Iwapo au la Dkt Ruto ataagiza mawaziri wake wakome kuingiliana, kile kitakachofuatiliwa sana ni jinsi watakavyoendesha majukumu tofauti katika wizara zao.

Ikizingatiwa kuwa Rais Ruto tayari ameteua Makatibu wa Wizara, ambao watasaidia Mawaziri katika masuala ya sera, baadhi yao wanaonekana kutojua kazi yao – la sivyo, migawanyiko mikali imeanza kutokea.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ NAIBU RAIS MWAMINIFU KWA RAIS? SIO KENYA



# MPANGO MKUU WA GACHAGUA

## Juhudi za Naibu Rais za kujaza pengo la uongozi eneo la Mlima Kenya baada ya Uhuru kuondoka ni msingi wa kutafuta urais siku za usoni

• Na MACHARIA GAITHO

Rais Rigathi Gachagua alipotangaza wazi kuwa aliwaelekeza wabunge kutoka ngome yake ya Mlima Kenya wamuunge mkono aliyekuwa Mbunge wa Kieni Kanini Kega kwa uchaguzi wa wawakilishi wa Kenya katika Bunge la Jumuia ya Afrika Mashariki (EALA), hangekuwa mjinga kutarajia kuwa Rais William Ruto hangetambua jambo hilo.

Alichokuwa akithibitisha hadharani Naibu Rais, ingawa si kwa maneno mengi, ni kuwa aliongoza wabunge wa Mlima Kenya katika muungano wa Kenya Kwanza kumkaidi Rais na kuunga mkono mgombeaji wa muungano wa Azimio unaoongozwa na Raila Odinga.

Ingawa Ruto na Gachagua wamepuuzilia mbali madai ya kuwepo kwa mgawanyiko na kushikilia kuwa Kenya Kwanza bado imeungana, mgawanyiko huo kuhusu uchaguzi wa EALA hauwezi kupuuzwa. Ni kieleleza cha tahuruki ambayo tayari imekijitokeza kati ya makabila mawili makubwa na ngome mbili kuu kuhusu masuala ya teuzi katika afisi kubwa serikalini zikiwemo Makatibu wa Wizara, Mawaziri Wasaidizi, teuzi za mabalozi, wakuu wa mashirika ya serikali na tume za kikatiba.

Ni wazi kwamba, anavyosema hadharani, Gachagua anaendeleza mchakato wa kushawishi jamii za Mlima Kenya, Wakikuyu na ndugu zao Wameru na Waembu, kuunga mkono serikali ya Ruto.

Jamii za Mlima Kenya ziliwapigia kura kwa wingi Ruto na Gachagua na kuuwezesha muungano wa Kenya Kwanza kushinda viti vyote katika eneo hilo lenye kura nyingi, lakini kuna wachache ambao bado ni waaminifu kwa rais mstaafu Uhuru Kenyatta ambao Naibu Rais anataka kuwavuta upande wake.

Kwa hivyo, kumsaidia Kega kushinda nafasi katika EALA, na kwa njia hiyo kumvuta upande wake, pamoja na kuwashawishi viongozi wakuu kutoka jamii ya Wakikuyu waliomuunga Raila kunaashiria mazuri kwa Kenya Kwanza. Hiyo hasa ndiyo mbinu anayotumia Ruto kummaliza nguvu Raila kwa kuvamia Azimio na kushawishi wabunge, magavana na viongozi wengine wa muungano huo kuvuka upande wa Kenya Kwanza.

Hata hivyo, tofauti ni kwamba njama ya Rigathi inaweza kufasiriwa kuwa inayolenga kuimarisha nafasi yake ya kisiasa ndani ya Kenya Kwanza na chama cha United Democratic Alliance (UDA), badala ya kuimarisha kuungwa mkono kwa utawala wa Ruto.

Wakati wa kampeni za urais, mbunge huyo wa zamani wa Mathira alijizuia katika majukwaa mbalimbali kutoa hakikisho kuwa, kama Naibu Rais, angekuwa mwaminifu na mtiifu kwa Rais; kwamba wajibu wake ungekuwa kufanya kazi kwa maagizo ya rais.

Mapinduzi yake wakati wa kura ya EALA yalithibitisha vinginevyo, na anapoendelea kuimarisha nafasi yake kisiasa, haiwezi kuwa tu kuimarisha kuungwa mkono kwa Rais Ruto katika Mlima Kenya, bali kujenga nafasi yake pia. Lengo la kufanya hivyo sio tu kuimarisha wajibu wake kama Naibu Rais, bali kujijenga ili yeye pia aweze kuwania urais miaka ijayo.

Alipotoa hakikisho kuwa atakuwa nambari

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## kurunzi ya kenya

mbili mtiifu na mwaminifu, lazima Gachagua alifahamu wazi kuwa Ruto kama Naibu Rais wa Uhuru Kenyatta, hakuwa mtiifu na mwaminifu. Alimaanisha kuwa hatakuwa Naibu Rais kama Ruto.

Muhula wa pili wa utawala wa Jubilee ulishuhudia tofauti za wazi kati ya Rais na naibu wake. Uhuru alivunja makubaliano ya urithi wa urais kwa kuungana na Raila chini ya Mpango wa Maridhiano, na hatimaye akaunga azma yake ya urais chini ya Azimio.

Ruto naye alimuasi na akaendeleza kampeni zake za urais na kufaulu kupenya ngome ya Uhuru ya Mlima Kenya, akiendeleza kauli mbiu ya maskini dhidi ya matajiri ambayo ilimgeuza naibu rais wa mihula miwili kuwa mgombeaji "kutoka nje" anayeongoza uasi dhidi ya wakuu serikalini.

Talaka ya Uhuru na Ruto ilionyesha mahusiano machungu zaidi kati ya rais na naibu wake tangu uhuru. Mahusiano ya Rais Jomo Kenyatta na waliokuwa Makamu wa Rais Oginga Odinga na Daniel Arap Moi; Rais Moi na waliokuwa makamu wake Mwai Kibaki, Josephat Karanja na George Saitoti, yote yalionyesha rais ambaye hangevumilia naibu wake mwenye nguvu anayejenga ngome yake ya kisiasa kwa lengo la kuwania urais wakati ukiwadia.

Hivyo ndiyo ilivyokuwa kwa Uhuru na Ruto lakini alidhibitiwa na Katiba ya 2010 iliyofanya uchaguzi wa urais kuwa mkataba usioweza kuvunjwa. Naibu Rais hakuwa mteule wa rais, bali alichaguliwa kupitia tiketi sawa na hangeweza kufutwa kazi.

Kama hiyo ndiyo ilikuwa shida ya Ruto kwa Uhuru, inaonekana ndiyo itakuwa shida ya Gachagua kwa Ruto anapojitahidi kujenga ngome ya kisiasa.

Kulingana na Kanini Kega, hatua yake ya kuunga mkono Gachagua baada ya kupata kiti cha EALA inatokana na haja ya kuisukuma serikali kutekeleza maendeleo katika eneo la Mlima Kenya. "Sitaki kutoa kauli kuhusu hilo kwa sababu mimi sio mfuasi wa mrengo huo wa kisiasa," akaambia Darubini ya Wiki.

Kuhusu iwapo kulikuwa na njama ya kisiasa katika UDA na Kenya Kwanza kumhusu Naibu Rais, anasema hajui na kuwa hayo hayamhusu kwa sababu uaminifu wake ungali katika chama cha Jubilee na Azimio.

Hiyo inaweza kuonekana kama kujikanganya, lakini Kega alisisitiza kuwa kukubali kwake kufanya kazi na Gachagua kunatokana na kutambua hali ilivyo sasa bali sio ishara kuwa anahama chama cha Uhuru cha Jubilee na kuacha kumuunga mkono Raila chini ya Azimio. Alisisitiza kuwa atabakia kuwa mwanachama mwaminifu wa Jubilee chini ya uongozi wa Uhuru na mkurugenzi wake wa uchaguzi, akishikilia kuwa ushirika wa chama hicho na Azimio na Raila bado ni thabiti.

Ukweli mpya, akasema, ni kuwa Ruto ni Rais na Gachagua ni naibu wake, kwa hivyo masuala yote kuhusu Mlima Kenya ni lazima yapitishwe kwa mtu mwenye cheo cha juu serikalini kutoka eneo hilo. Hiyo ilimaanisha kutambua nafasi ya Gachagua na kuwezesha Mlima Kenya kuzungumza kwa sauti moja kutetea rasilimali za maendeleo na masilahi mengine. "Tunaweza tu kutumia mtu mmoja serikalini na huyo ni Naibu Rais," akasema, na kuongeza, "Hatujafikia siasa za 2027" kuhusu uchaguzi mkuu.

Alieleza kuwa Jubilee hufanya maamuzi yake kupitia taasisi stahiki, na tangu uchaguzi uliopita haijakutana kuhakiki uanachama wake ndani ya Azimio, kwa hivyo, hali haijabadilika. Lakini hiyo inaacha wazi uwezekano wa Jubilee kubadilisha nafasi yake katika Azimio.

Hata hivyo, inafaa kuzingatiwa kuwa viongozi wakuu wa Azimio katika Mlima Kenya kama vile Kega na aliyekuwa Mbunge wa Nyeri Mjini Ngunjiri Wambugu, wanaosema watafanyakazi na serikali, wanamuunga mkono Gachagua, badala ya kuunga mkono serikali ya Ruto. Je, wanatofautisha kati ya Rais na naibu wake? "Hapana, Hapana, Hapa," anajibu Kega akisema kuwa watafanyakazi na Ruto katika kuendeleza maslahi ya Mlima Kenya.

Kwa mfano, anasema, kama mwanachaa wa bunge la EALA, atawakilisha maslahi ya Kenya yatakavyobainishwa na serikali inayoongozwa na Ruto. Alieleza kuwa atakuwa akitangamana na Ruto na Gachagua kwa namna tofauti, Ruto kama Rais kuhusu masuala ya kitaifa katika EALA na Gachagua kuhusu masuala ya maendeleo ya Mlima Kenya.

Ukweli ni kuwa, hata hivyo, haja ya Gachagua kujaza nafasi ya uongozi wa Mlima Kenya iliyobaki wazi baada ya kuondoka kwa Uhuru, inahusu kujenga nafasi yake katika serikali hii na pia inahusu nia yake ya kuweka msingi wa kuwania urais miaka ijayo. Kulingana na Wambugu, ni sawa kwa Naibu Rais kuimarisha nafasi yake katika Kenya Kwanza ili awe na nguvu kujikuza kando na Ruto katika uchaguzi wa 2027.

Hili si jambo geni kwa sababu katika siasa za Kenya muhimu ni kutumia njia zozote zile kutambuliwa. Maandamano aliyozungumzia Raila yote ni sehemu ya mbinu za utetezi wa kisiasa, Wambugu anasema, akiongeza kuwa kiongozi huyo wa upinzani ametumia mbinu hiyo miaka ya nyuma kupata nafasi katika serikali za Uhuru, Kibaki na Moi.



Aliyekuwa Rais Uhuru Kenyatta

Anataja jinsi Mkuu wa Mawaziri Musalia Mudavadi na Spika wa Bunge la Kitaifa Moses Wetang'ula wanatetea nafasi zao wenyewe kwa kupinga nia ya UDA kupenya ngome yao ya Magharibi mwa Kenya katika uchaguzi mdogo wa useneta Bungoma. Wambugu pia anasema sasa anamuunga mkono Gachagua kwa sababu ni Naibu Rais, na ataunga mkono mtu mwingine yeyote katika nafasi hiyo atakayeendeleza maslahi ya Mlima Kenya.

Hiyo ina maana anamuacha Raila? Anajibu kwa kusema la, lakini akibaini kuwa hakuwa mtu wa Raila, bali mtu wa Uhuru aliyekuwa akiunga azma ya urais ya Raila. "Tulifanya kadri ya uwezo wetu, tukapoteza na kwa sababu uchaguzi umeisha, hatuwezi kufanya chochote kuhusu hali hiyo."

Alidhani Raila alifaa zaidi kuendeleza maono ya Uhuru, lakini ukweli ni kuwa hilo halikufanyika na Jubilee inafaa kukubali hali hiyo mpya. Uhuru, anasema ametambua hali hiyo na anashughulika na wajibu wake mpya kama mpatanishi wa amani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa hivyo ni lazima viongozi wa Mlima Kenya washirikiane na walio serikalini kuendeleze ajenda zao. "Ukweli mpya ni kuwa Ruto ni Rais na Rigathi ni Naibu Rais na nafasi hiyo inamfanya kiongozi wa Mlima Kenya mwenye hadhi ya juu zaidi serikalini. "Miradi ya maendeleo tuliyodhani tungefuatilia chini ya serikali ya Raila sasa itabidi ifuatiliwe chini ya Rais Ruto," anasema Wambugu.

Kwa hivyo, suala ni kuunga mkono Gachagua badala ya Ruto? Wambugu apuuza hilo kuwa swali lisilo na maana. Kulingana naye, hoja si kuhusu mmoja wa wawili hao kwa sababu nafasi wanazoshikilia zingechukuliwa na watu wengine, lakini uhalisi wa ushindani wa kisiasa nchini ambao hutegemea zaidi maslahi ya kikabila na kimaeneo.

Wambugu anakubali kuwa Naibu Rais hana budi kujiimarisha, akifahamu fika kuwa hakuwa chaguo la kwanza la viongozi wa UDA kutoka Mlima Kenya. Hasa, ni wazi kuwa huku wanaohama kujiunga na Kenya wakionyesha ishara ya kuunga mkono Gachagua, wengine wengi waliokuwa na Ruto tangu mwanzo na ni watiifu kwake, wanaonekana kutovutiwa kwa Naibu Rais.

Viongozi kama Mbunge wa Kikuyu Kimani Ichung'wa, Mbunge wa Kiharu Ndindi Nyoro na mawaziri Moses Kuria (Biashara), Mithika Linturi (Kilimo) na Kithure Kindiki (Usalama) huenda hawatasema wazi, lakini wanahisi Gachagua aliingia kambi ya Ruto baada ya wengine waliokuwa naye (rais) kwa muda mrefu.

Kwa hakika Kindiki, alimshinda Gachagua katika uchaguzi wa ndani wa nafasi wa mgombea mwenza. Lakini Profesa Kindiki alilazimika kukubali uamuzi wa Ruto wa kumteua Gachagua, ingawa shingo upande. Rais na Naibu Rais hawana budi ila kufanya kazi pamoja angalau kwa miaka mitano ijayo.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# habari kwa picha



Picha ya kutoka angani ikionyesha maandamo yaliyoongozwa na Rais wa Mexico Andres Manuel Lopez Obrador katika jiji kuu la nchi hiyo kuadhimisha miaka minne ya utawala wake mnamO Novemba 27. PICHA I AFP




Chombo cha kufyatua makombora mengi kwa wakati mmoja kikifyatua makombora kuelekea maeneo ya Urusi kwenye mstari wa mbele karibu na Bakhmut, eneo la Donetsk, katika vita kati ya Urusi na Ukraine. PICHA I AFP



Makao ya msituni ya 'Poste des Mines' katikati ya msitu wa miti ya misonobari eneo la Le Chenit. Msitu huo umejaa miti ya misonobari ambayo imekuwepo kwa mamia ya miaka na imefunika mpaka kati ya Ufaransa na Uswizi. PICHA I AFP



Waigizaji wakishiriki maonyesho wakati wa Tamasha katika jiji la Dakar mnamo Novemba 26. Tamasha hilo huandaliwa jijini humo kila Novemba kusherehekea urithi wa kitamaduni huku watu kutoka kote nchini wakionyesha mavazi yao ya kitamaduni. PICHA I AFP



Aliyekuwa Rais Uhuru Kenyatta, Msimamizi wa mashauri ya amani yanayoongozwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) jijini Nairobi, Rais wa Burundi, Jenerali Évariste Ndayishimiye (kulia) na Rais William Ruto wakifika kwa ufunguzi rasmi wa Awamu ya Tatu ya Mashauri ya Amani kati ya Wakongo katika mkahawa wa Safari Park mnamo Novemba 28. PICHA I AFP



Behewa la mradi wa reli ya kisasa (SGR) likitolewa katika meli baada ya Tanzania kupokea mabehewa 14 ya nauli nafuu kutoka kwa kampuni ya Korea Kusini ya Sung Shin Rolling Stock (SSRT) katika bandari ya Dar es Salaam mnamo Novemba 25. Shirika la Reli Tanzania litaanza kutumia sehemu ya kwanza ya reli hiyo ya karibu kilomita 300 kati ya Dar es Salaam na Morogoro kuanzia Januari 2023. PICHA I AFP



Nyumba iliyoharibiwa mjini Bakhmut, eneo la Donetsk, mnamo Novemba 29 katika vita vinavyoendelea kati ya Urusi na Ukraine. Bakhmut, ambao wakati mmoja ulijulikana kwa mashamba yake ya mizabibu na migodi ya chumvi sasa umepewa jina "kinu cha kusagia nyama" kutokana na vita vya zaidi ya miezi sita vya kutumia makombora na makabiliano ya risasi katika juhudi za kudhibiti mji huo. PICHA I AFP

Nation Media Group "ePaper Copy"

Jukwaa La

# Vijana



# FUNDI WA RAIS

*Ashok Sunny ni mtaalamu wa suti za kifahari zinazoundwa kwa vitambaa vya ubora wa juu zaidi na kushonwa kwa mikono*

NAFASI YA VIJANA

# TUNAWEZA KUZIMA WIZI WA MIFUGO

**Ni magaidi?** Wezi wa mifugo siku hizi hawatafuti idhini ya wazee kabla ya kuvamia jamii jirani

● NA DOMINIC PKALYA

Siku chache zilizopita, visa vya wizi wa mifugo na ujangili vimeongezeka katika maeneo kame. Watu wameuawa, mali (mifugo) kuibwa, biashara kuvurugwa na taasisi za masomo kufungwa.

Maeneo ya Bonde la Ufa - Kaskazini na Mashariki ya Juu - ndiyo yameathirika zaidi, hali iliyolazimisha wanasaisa na jamii kushinikiza serikali kuwachakulia wezi wa mifugo na majangili kuwa magaidi.

Maana ya presha hii ni kuwa kitambulisho cha ugaidi hatimaye kitaruhusu serikali na jamii ya kimataifa kutumia nguvu kali kukabiliana na washukiwa. Kinaweza kuifanya serikali kutumia vikosi na silaha maalumu, likiwemo Jeshi la Ulinzi la Kenya (KDF).



Wakati wa mkutano wa usalama hivi majuzi katika Kaunti ya Samburu, Waziri wa Usalama Profesa Kithure Kindiki alikubaliana na shinikizo hizo aliposema wizi wa mifugo na ujangili ni sawa na ugaidi. Hasa, alisema hakuna tofauti kati ya wezi wa mifugo na Al Shabaab.

Wezi wa mifugo wamesababisha uharibifu na mateso makuwa kwa Wakenya, hasa katika maeneo kame (ASALs). Hii ndiyo maana Wakenya wameunga mkono juhudi mpya na kujitolea kwa serikali kukomesha kabisa tishio hilo.

Hata hivyo, kuwachukulia wezi wa mifugo kuwa magaidi sio suluhisho la kudumu kwa uhalifu huu wenye historia ndefu.

Shida ya kuchukulia wizi wa mifugo kuwa ugaidi inaanza na maana ya ugaidi. Hakuna maana ya kisheria ya ugaidi inayokubalika na wote. Sheria yetu ya Kuzuia Ugaidi (POTA) ya 2012 haitoi maana kamili ya ugaidi au gaidi. Inafafanua maana ya kitendo cha kigaidi, kundi au mali. Sheria hiyo inaendelea kuelezea "mafunzo ya kigaidi" kwa mtazamo wa kiitikadi na imani.

Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ugaidi unatoa maana ya ugaidi kwa kuangazia "vitendo vya kigaidi" vilivyoanishwa na sheria ya POTA. Mkakati huo pia unaelezea "shirika au kundi la kigaidi" kuwa, miongoni mwa mengine, makundi yenye uongozi na udhibiti wa kuendeleza propaganda na itikadi kali".

Kwa kutumia maelezo haya, ni wazi kuwa wezi wa mifugo na majangili, hawaungi mkono au kuendeleza, kupitia vita na propaganda, itikadi fulani kali au imani. Magaidi wa sasa huwa hawatafuti idhini kutoka kwa wazee kabla ya kushambulia kabila jirani au jamii.

Wezi wa mifugo na majangili wa kisasa wameacha muundo wa uongozi wa kitamaduni na ngazi za uongozi. Kwa hivyo, kuchanganya wizi wa mifugo na ugaidi sio suluhisho.

Kama serikali haiwezi kupambana na majangili wasio na mafunzo maalumu, inawezaje kupambana na magaidi walio na itikadi kali kama Al-Shabaab wanaoendelea kupata maeneo mapya Afrika Mashariki ya kuwawezesha kujipanga upya, kujifunza na kusajili wafuasi zaidi?

Tukifaulu kuwachukulia wezi wa mifugo kuwa magaidi basi kingine ambacho tunaweza kufanya ni kuchukulia uhalifu mwingine wowote unaoweza kukabiliwa chini ya Sheria ya Uhalifu kuwa "vitendo vya kigaidi".

Wezi wa mifugo na majangili wanaweza kudhibitiwa kwa kutumia vyombo vilivyoko vya kisheria, kisera na kiusumamizi. Kile ambacho kimekosekana ni nia njema ya kisiasa katika ngazi za kitaifa na zile za kaunti kushughulikia shida hii.

Utafiti unaonyesha kuwa nyakati nyingi, maafisa wa polisi wanaotumwa kuwafurusha wezi wa mifugo, kukomboa mifugo na kutwaa silaha haramu huombwa na viongozi wa kiraia wasitekeleze operesheni hizo kikamilifu.

Kuruhusu vikosi vya usalama kufanya kazi yake bila kuzuiwa, kuendesha elimu ya kimsingi ya lazima, kuwekeza katika elimu na kushirikisha chumi za maeneo ya ASAL katika uchumi wa kitaifa ndilo suluhisho la kudumu.

Bw Pkalya ni mchanganuzii wa masuala ya mizozo.

Maoni yoyote kuhusu masuala makuu? Tungependa kusikia kutoka kwako. Tuma maoni yako kwa: ***weeklyreview@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

## WANAVYOSEMA



**Millicent Naserian**

Naibu Rais Rigathi Gachagua anapaswa kuongoza Wakenya katika kupata suluhisho bora.

Maslahi ya watu yanafaa kuja kwanza, badala ya miradi ambayo haina manufaa katika jamii.

Serikali inafaa kujikaza kupunguza ubadhirifu wa pesa na itenge pesa kwa mahitaji ya dharura, kama vile kutoa msaada wa chakula na kufadhili miradi ya kupunguza makali ya ukame.

*- Kiongozi wa vijana*



**Natalie Wafula**

Pendekezo la Naibu Rais la kubuni hazina ya kitaifa kukabiliana na makali ya kiangazi haliwezi kufaulu kwa sababu Wakenya wengi hawana pesa za kugharamia mahitaji ya kimsingi. Hii inaonyesha serikali haijawa tayari kutimiza ahadi ambazo Kenya Kwanza ilitoa. Nchi inapoendelea kuchukua mikopo zaidi, ni lazima kuwe na uwajibikaji kuhusu jinsi pesa hizo zinavyotumiwa.

*- Mwanafunzi, MKU*



**Maxwell Munyendo**

Hatua ya serikali na mashirika kadhaa za kutoa chakula kwa walio na njaa ni nzuri. Lakini napinga wazo la Naibu Rais Rigathi Gachagua la kusambaza nambari ya kutuma pesa (Paybill) za mchango kwa hazina ya kitaifa ya kupambana na njaa. Pesa hizo hatimaye hutumiwa vibaya au kuibwa, na hivyo kukosa kutimiza malengo yake.

*- Mchanganuzi wa masuala ya utawala*



**Nickson Mtai**

Serikali inafaa kusaidia watu walio na njaa, hasa katika maeneo kame nchini kwa kununua mahindi kutoka kwa wakulima kwa bei iliyokubaliwa kisha kuyasambaza kwa waathiriwa. Hatua hiyo itapunguza athari za ukame.

*- Mkurugenzi wa Mipango, Muungano wa Wanafunzi wa zamani wa Vyuo Vikuu na Vyuo kutoka Kiambu*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

MTAZAMO WANGU



# MWALIMU WA KENYA AMECHEZEWA SHERE

**Watoto likizoni:** Ni wakati huu ambapo Wakenya huanza kugundua umuhimu wa shule na walimu, na zaidi, hali yao ya akili



**Watoto wakati wa likizo wakicheza kwa tawi la mti ulioanguka katika kijiji cha Mukur, eneo la Tiaty, Kaunti ya Baringo, huku mmoja wao (kulia), akimbeba mwenzake mnamo Desemba 22, 2021.**
PICHA | JARED NYATAYA

• NA MOSES OJUANG'

Kalenda ya masomo ambayo iliyovurugwa na kufungwa kwa shule kutokana na janga la Covid-19 inarudi hali ya kawaida. Kwa mitihani kufanyika katika mazingira tulivu, wanafunzi wengine wote tayari wako nyumbani na wameanza kuwa wasumbufu kwa wazazi wao. Ni wakati huu ambapo Wakenya huanza kubaini umuhimu wa shule na walimu, na zaidi, hali yao kiakili.

Ni wakati huu pia ambapo kila kitu kuhusu wizara ya elimu hujulikana. Ni wakati ambapo kila mfanyakazi wa ngazi za juu serikalini mwenye uhusiano na wizara hiyo; kila afisa wa kiwango cha kati mwenye uhusiano wowote na Baraza la Kitaifa la Mitihani (KNEC) hutoka katika afisi zao. Ni wakati wao kuambia vyombo vya habari na yeyote ambaye atawasikiliza, kuwa huwa wanatekeleza majukumu muhimu sana katika elimu ya watoto wao. Ni wakati wa watu wacheshi.

Hasa, mtu anaweza kushawishika kudhani kuwa bila maafisa hao, hakuna lolote lingefanyika kama ilivyotarajiwa. Kwa sasa wanajitokeza sana kuinua nyuso zao kuonyesha jinsi walivyo muhimu katika jamii na majukumu mazito wanayotekeleza.

Tayari, habari zimeenea katika vyombo vya habari na wataangaziwa katika muda wote ambao mtihani huo utaendelea. Walimu wasio na uwezo ambao watatumiwa kutekeleza majukumu madogo na yasiyo muhimu kana kwamba hawangetayarisha wanafunzi kwa miaka hiyo yote bila mwongozo wa maafisa hao.

Katika wiki tatu zijazo, walimu hao hawatakuwa na amani. Ndio watakuwa katika kila sehemu nchini wakisimamia mtihani huo, ambapo baada ya kazi hiyo ngumu, watatumwa katika shule tofauti za upili kwa wiki tatu kusahihisha karatasi hizo. Mchango wao hautakuwa muhimu kwani hawatakuwa wakionekana sana.

Wakati pekee ambao huenda wakaangaziwa katika mchakato huo ni pale kosa dogo linapotokea wakati wa usahihishaji wa mtihani. Kwa sasa, KNEC, maafisa wa Wizara ya Elimu na Tume ya Kuajiri Walimu (TSC) wameungana kumsimamia mwalimu. Kuna pengo fulani, kwani ni vigumu kumjua mwajiri wa mwalimu. Kila afisa anayepiga kelele ana mamlaka kumhangaisha na kumkasirisha mwalimu.

Hili limekuwa likiendelea kwa muda mrefu sana huku miungano ya walimu, ambayo lengo lake ni kufaidika kwa ada kutoka kwa mishahara ya walimu ikinyamaza kana kwamba mambo haya hayaihusu sikio wala ndewe.

Mtindo huu umekita mizizi, hasa wakati wa usimamizi wa mitihani, kwa kiwango ambacho walimu wengi wanaochoka hujitoa katika shughuli hiyo. Tatizo ni kuwa, bila kujitolea kwao, hakuna mtihani unaoweza kufanywa. Siku hizi, inabidi walazimishwe kufanya kazi hiyo waliyokuwa wakipigania miaka ya hapo awali. Wanahitajika sana kiasi kuwa inabidi washinikizwe kufanya kazi hizo zisizowaridhisha.

Wakati huo huo, kuna washukiwa wakuu kila wakati kunapokuwa na visa vya wizi wa mitihani! Na kufikia mwisho wa shughuli hii, kutakuwa na walimu wengi katika vizimba vya mahakama zetu wakishtakiwa kwa kila aina ya makosa. Ni hali ambayo imekuwa ikishuhudiwa kila mwaka na inaendelea kuwa mbaya.

Maslahi ya mwalimu Kenya hayajashughulikiwi ipasavyo. Taifa ambalo haliheshimu walimu wa watoto wake limebaki nyuma katika masuala ya utamaduni; nchi ambayo haijui kosa inalofanya kuhusu mustakabali wake; taifa ambalo linahitaji mwanzo mpya.

Kunapozuka matatizo yoyote, kunapaswa kuwa na sera kuhusu jinsi yanafaa kushughulikiwa. Onyo zinazotolewa kwa walimu kutoka ofisi hiyo zinawaaibishwa na kuwadunisha machoni mwa jamii.

Baada ya mtihani kukamilika na Waziri kusifiwa akitangaza matokeo, walimu watarudi madarasani kutayarisha watahiniwa wengine. Walimu ambao shule zao hazitakuwa zimefanya vizuri bado watalaumiwa na maafisa wa elimu kutoka wizara hiyo.

Malipo ya wote waliojinyima muda wao ili kushiriki katika shughuli hii muhimu yatatolewa Aprili, kulingana na hali itakavyokuwa katika KNEC. Lazima mambo yabadilike mwaka huu, la sivyo tunajitafutia tatizo kubwa siku za usoni.

Bw Ojuang ni mchanganuzi wa masuala ya kijamii

**mojuang@gmail.com**

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

VIWANDA VIDOGO

# KUONGEZEA LADHA

**HEBU TUZUNGUMZE KUHUSU MLO:** Piquant Spices imejituma kufanya upishi kuwa ufundi badala ya kazi ya nyumbani, ikitengeneza viungo vinavyoweza kutumiwa na familia nzima

• NA EDDY ASHIOYA

Watu wengi hawakubali wanapofeli lakini kilichojitokeza wazi katika saa moja au zaidi ya mazungumzo yangu na Stephen Machua, mwanzilishi mwenza wa Piquant Spices, ni kuwa kufeli, kwa kutegemea unavyokutazama, au unakutazama ukiwa na nani, kunaweza kuwa kizingiti au kichocheo cha ufanisi. Kufeli pia kuna vyanzo vingi. Naweza kufikiria sababu 250,000 kwa sababu hizo ndizo pesa ambazo Machua na mwanzilishi mwenza, SK Kamau (ambaye alihudumu kama mpishi kwa muda) walipoteza katika juhudi za kutaka kufanikiwa.

"Tulianza kwa kilimo cha nyanya na ndizi kwa sababu tulitaka kusoma mchakato mzima wa uzalishaji. Tuliwekeza Sh250,000 lakini tukapata mavuno ya Sh9,000". Hii hata si asilimia tano, ninamwambia. Hasa, hiyo ni asilimia 3.6 pekee! "Kupoteza 250,000 si mchezo au si kitu kidogo."

Kufeli pia ni kitu cha kushangasha. Kwa upande mmoja, kunamaanisha umejaribu, kwa upande mwingine, ni uamuzi kuwa hutoshi kamwe, sio tu kutoweza. "Tuligundua kuwa, ingawa tulikuwa tukilima eneo lisilo na gharama kubwa kwa uzalishaji wa ndizi, hakukuwa na soko kubwa la unga wa ndizi. Kisha tukafikiria kuwa, kwa sababu tulikuwa tumetoka mbali, pia tungejaribu viungo."

Unafaulu katika jaribio la tatu? Pengine - tutazungumzia hilo.

Kwanza, mtu anajuaje ni mzuri kwa viungo? Machua anatoa ishara ya mjasiriamali shupavu (au ni mwamuzi?) ambaye haamini katika kuwapa watu kitu walicho nacho nyumbani. "Lazima tungetafuta kitu tofauti. Tulifanya utafiti na tukagundua watu hawakuwa wakitumia viungo kwa sababu familia ya kawaida hutaka kuwa na chungu kimoja cha chakula. Unapotaka kutumia viungo, unataka kiungo kinachoweza kutumiwa na kila mtu katika familia. Na pia watu wengi hupata kiungulia wakitumia viungo, hasa kwa sababu viungo huwa havijaoshwa vyema au kukaushwa."

Wakitumia mawazo hayo mawili ya kipekee ya uuzaji, wangeweza kufanya walichotaka, na walikuwa tayari kukiongeza ladha. Walianzisha Piquant Spices, kazi yake ikiwa ni kufanya upishi kuwa ufundi badala ya kazi ya kawaida ya nyumbani. Piquant, kwa muundo au mjadala, inamaanisha "kitu kinachosisimua akili". "Kazi yetu ni kuhakikisha viungo vinaweza kutumiwa na familia nzima."

Ananiambia sasa wanatengeneza kiungo chao cha tano, wakiwa wamepeleka viungo vyao sehemu nyingi nchini, wakitumia habari wanazopokea kukidhi mahitaji ya watu. Maoni, walisema wahenga, ni kama pua; kila mtu ana yake. Hasa inapohusu chakula, au ladha yake.



Kutoka kulia: Stephen Machua, mwanzilishi-mwenza wa Piquant Spices, Pedro Sanchez, Waziri Mkuu wa Uhispania, na Balozi Kirimi Kaberia, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda, wakiwa katika Taasisi ya Utafiti wa Ustawi wa Viwanda Kenya mnamo Oktoba 26.

Kupima viungo, mtu anajifunza kwa haraka, kunahitaji umakini mkubwa kama wa mtengenezaji wa glasi na usahihi wa kisu kwa mshipa. Kwa kufahamu maelezo ya Uhusiano Mwema kutoka kwa mpishi - hii ni bora na yenye ladha, hii tata lakini makinifu - Piquant Spices imependwa na watumiaji.




Baadhi ya viungo vya Piquant.

Pilau Masala ndiyo wanauza kwa wingi, haitulii kwenye rafu kama, naam, kiungo kizuri. Huku msimu wa sherehe ukikaribia, pesa katika akaunti ya Piquant Spices zinaendelea kuongezeka. "Pilau Masala ni maarufu sana na hiyo huenda ni kutoakana na kurejea kwa hafla na sherehe."

"Tumepata masoko Uganda na Tanzania, hasa Arusha na Moshi." Cha kufurahisha ni kuwa, anasema, soko lao la kanda ni kubwa kuliko soko la humu nchini. "Biashara inalipa bili zake yenyewe." Bili hizi zinajumuisha gharama ya kuendesha biashara na mishahara ya wafanyakazi tisa, wakiwemo saba ambao ni

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kibarua. "Katika Arusha na Moshi, tuna karibu maduka 30. Hapa Kenya bado tunatafuta wasambazaji na tumekuwa tukiuza kupitia kwa mtandao."

Hivi majuzi walianza kusambaza Kiambu na eneo la Voi hadi Mtwapa; eneo lingine ni Ruiru hadi Githurai, na pia maduka kadhaa mjini Nakuru.

Mbali na Pilau Masala, Piquant ina viungo vingine viwili katika soko: Tea Masala, Pilau Masala na Viungo Mseto, na vingine kumi vinavyosubiri kuidhinishwa na Shirika la Kukadiria Ubora wa Bidhaa Kenya: Curry Powder, Beef Masala, Chicken Masala, Paprika, Turmeric, Black Pepper, Cinnamon, Cardamom, Ginger na Garam Masala.

Kwa wakati huu, wanatoa mali ghafi yao kutoka soko la Marikiti jijini Nairobi na pia Kisii, Kiambu, Uganda na Tanzania.

"Kufikia sasa, tangawizi kutoka Uganda imekuwa thabiti kwa uwezo. Awali, tulikuwa tukiipata kutoka Kiambu na Kisii." Tatizo la tangawizi ya Kenya, anasema, ni kuwa si thabiti, iwe ni kwa bei au ubora.

Kwa kutazama nyuma kuhusu kazi yake, anaeleza kuwa matukio ambayo yalimsukuma hadi akafika alipo leo. "Nilijua nilitaka kujiunga na utengenezaji wa bidhaa. Niliishi Uingereza na nikaenda kusomea Canada. Lakini kula vyakula vyao visivyo na ladha na kutegemea viungo kuongeza ladha kulinichochea zaidi."

Anasema biashara hiyo inakua lakini uwezo wa kupata mashini, hasa ya kukausha, ni changamoto, ikizingatiwa kuwa wamepewa eneo la kufanyia kazi katika Taasisi ya Utafiti na Ukuzaji wa Viwanda ya Kenya. "Ukiwa katika eneo la kupewa unamtegemea mtu mwingine. Kwa mfano, ninafanya kazi ya kutengeneza bidhaa wiki hii, kwa hivyo najua nitapata nafasi nyingine Machi, na hii ni kwa sababu sehemu mbadala za kibiashara ni ghali mno."

"Na bila shaka kupatikana kwa soko ni changamoto pia. Hatuna mtaji mkubwa na iwapo kila mtu atataka bidhaa kwa mkopo, basi uzalishaji utakwama." Kama ningepewa nafasi ya duka kubwa leo, anasema, na nilipwe baada ya siku 120, inamaanisha nitakuwa na pesa nyingi zimefungwa (ambazo ningetumia) kutengeneza bidhaa kwa wateja wengine.

Ujasiriamali Kenya, hasa kwa kijana, ni mtego unaoweza kufyatuka. "Sekta ya utengenezaji haikuanzishwa kwa watu wasio na uwezo." Walipoanza kutafuta mbinu za upakiaji, walikuwa wakipata zilizo ghali sana. "Tunashukuru tuliweza kupata watu waliofanya kazi nasi katika kiwango tulichokuwa." Na, ni lazima isemwe, Machua na Kamau walishinda changamoto, lakini sio kabla ya kuzama tayari ambapo tajiriba waliyopata kupitia moto wa chuma iliwafanya wastahimilivu.

Kwa uaminifu wa dhati, Machua anasema ujasiriamali umejenga ustahimilivu wake. Anaendelea kunisimulia jinsi mmoja wa wateja wake alimuahidi makuu, kisha akajiondoa dakika ya mwisho na kumuacha katika hali mbaya. Lakini washindi hawana visingizio na kwa njia moja, alipata suluhu.

"Ujasiriamali unakulazimisha kufikiria kwa haraka." Lakini pia anaoekana kuwa mtu wa kubadilika, mtu aliye kwenye safari anayeendelea kujijenga. Kwa sababu hivyo ndivyo inahitajika kujenga biashara - jasho na mfupa, damu na uchungu. Hii ndiyo lugha ya mchapakazi.

Alifikaje hapa? "Ni sadfa, fursa na nafasi. Haikuwa kwa kutaka kwa sababu ilifanyika tulipokuwa tumeomba ruzuku na tulikuwa tumesubiri kwa miaka miwili. Hatukuwa na hakika kama tungeipata."




Ruzuku anayozungumzia ni ruzuku ya biashara kutoka shindano la Mpango wa Biashara la MbeleNaBiz la 2019 (mpango wa serikali wa Kenya chini ya Mradi wa Kuwezesha Vijana wa Kenya).

Alikuwa amerudi kutoka Canada baada ya kuhitimu digrii ya Uzamili katika Sera ya Umma katika Chuo Kikuu cha Calgary kuongezea Digrii ya Uzamili katika Sayansi ya Ustawi na Mipango ya Miji kutoka Chuo Kikuu cha Manchester.

"Ujasiriamali unakufunza uaminifu." Uaminifu ni kitu muhimu katika sekta hii. Kuachia mtu majukumu, anasema, hakufanyi kazi miaka ya mwanzo. Lazima uwe hapo. Lazima ufike. Anazungumza kama mfuasi wa maadili ya Lombardi.

Kwa Vince Lombardi, anayetajwa kama mwanasoka shupavu, ushindi kwa kila hali, na kwa gharama yoyote, ndicho kitu muhimu. Ushindi ni tabia. Inasikitisha, kushindwa pia ni tabia."

Huwezi kuthubutu kufanya makosa. Hasa wakati uko katika sekta ya chakula. Baadhi ya watu wanaweza kutumia njia za mkato na hii inaweza kuharibu chapa yako."

Anashukuru familia na ujuzi wa maisha kwa kumtia motisha. Sio tu kama sehemu yake, lakini pia wamechangia kufaulu kwake. Msimu wa maisha ambao yuko kwa wakati huu ni upi? "Ni wa kutengeneza pesa na kuunda nafasi za ajira kwa wengine."

"Furaha," anasema, "ni kuweza kuona nikipiga hatua inayofaa. Hata kama ni hatua ndogo. Na kuwa na afya nzuri," anachukia kukwama, na maendeleo sio kuhusu pesa kila wakati.

Kwa Piquant, ufanisi ni kuwa jina kubwa. 'Lakini pia tuna ufanisi wa kila siku ambapo tumebadilisha wasioamini viungo kuwa waumini."

Je, mambo yamekuwa alivyotarajia mwanafunzi huyo wa zamani wa Chuo Kikuu cha Kiufundi cha Kenya mwenye umri wa miaka 31 alikohitimu na digriii ya Biashara (fedha)? "Kusema kweli la. Nafikiri nilitaka kuwa katika sera ya umma. Na mipango ya serikali. Lakini sasa niko katika jua kali."

Na hata hivyo, halalamiki. Anasema watu hawamuelewi. Oh, nani? Watu hufikiria mimi ni tajiri sana. Naam, wewe ni tajiri? "Nitakuwa mmoja." Je, mtu anawezaje kufika aliko leo? "Ninalinda na kutumia vyema urafiki. Ili kujenga soko la Tanzania, nililazimika kutumia marafiki kadhaa."

Hii inanielekeza moja kwa moja kwa swali linalofuata. Ni nini anachojua ambacho ninafaa kujua? "Unahitaji kumjua Mungu." Ni muumini tena wa dhati. "Ninahusisha ufanisi wa maisha yangu na maombi. "Watu hutuma watu kwetu. Ni Mungu tu."

Miongoni mwa viungo vyake, angetaka kuwa nini? Tea Masala, anasema. "Ina harufu nzuri ya kipekee ambayo inakuvutia kutoka mbali. Ni tamu na inapatikana." Kufeli pia kuko, kunapatikana na kunafaa. Na kwa nini isiwe hivyo? Kwa sababu kufeli, unakokufiria sana, ndiko kiungo cha ufanisi.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

## UKWELI

**Piquant Spices imeajiri watu saba**

Piquant ilianzishwa baada ya kushinda ruzuku ya biashara katika shindano la Mpango wa Biashara la MbeleNaBiz la 2019 (mpango wa serikali ya Kenya chini ya Mradi wa Kuwezesha Vijana wa Kenya).

Shehena yake ya kwanza Januari ilipelekwa London na ilikuwa kilo 75 walizoanza nazo.

Kabla ya kuanza kutengeneza viungo, Stephen na Kamau walipata mafunzo katika Taasisi ya Utafiti na Ukuzaji wa Viwanda Kenya, ambayo kwa wakati huu imewapa makao kwa mpango wa kuwakuza. Hapo ndipo wanatengenezea zao.

Mkebe wa gramu 50 unauzwa kwa Sh110 huku pakiti ndogo ya gramu 20 ikiuzwa kwa Sh20.

Stephen Machua amepokea tuzo kadhaa na ufadhili wa masomo zikiwemo African Leaders of Tomorrow (2019), Chevening Award (2018), UNLEASH Silver Award (2017), na UN-Habitat Emerging Community Champion (2016).

Machua pia ni Mhasibu aliyehitimu (Kenya) na mwanachama wa Taasisi ya Wataalamu ya Usimamizi wa Umma ya Canada.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

FASHONI NA UBUNIFU

# JINSI YA KUJIPAMBA

**MTINDO:** Ashok Sunny ni mtaalamu wa suti za kifahari za vitambaa vya ubora wa juu zinazoshonwa kwa mikono

NA SINDA MATIKO

Alipomsindikiza binti yake Mei iliyopita kumuoza kwa daktari raia wa Nigeria Alexander Ezenagu, Rais William Ruto alikuwa amejipamba si haba. Katika karamu hiyo ya kifahari iliyohudhuriwa na wageni mashuhuri pekee walioalikwa katika makao yake mjini Karen, Ruto nusura avunje shingo za watu waliogeuka kumtazama huku amejipigilia suti nyeusi ya aina yake, tai fupi nyeusi, viatu vyeusi, kofia nyeusi na bakora nyeusi. Shati jeupe la mikono mirefu lilitofautisha rangi na kukamilisha taswira hiyo ya kuvutia.

Mavazi hayo yalivutia watu mitandaoni, huku wengi wakitaka kijua aliyempamba. Imeibuka kuwa aliyehusika na mavazi ya kuvutia ya Ruto ni msanii wa mavazi na mwanamitindo Ashok Sunny, 32.

Kufikia leo, ineonekana, mbinu za tangu jadi zinazorudi nyuma karne kadhaa karibu na 1538 zinatumika kuunda suti za kifahari. Huku fasheni na mitindo ya mavazi ikibadilika, mtindo wa utendakazi unasalia vilevile: kuanzia hatua ya mwanzo kabisa, vipimo vya mteja na umbo vinachorwa kwenye karatasi ya rangi ya hudhurungi kwa kutumia kipimo cha mkanda, kipimo mraba, chaki na jicho makini sana.

Suti hiyo kisha inakatwa na Sunny au mmoja wa mafundi wake 20 na vazi la kwanza la vipimo linaundwa (suti hiyo huunganishwa kwa muda kwa kutumia uzi mweupe wenye gundi ili mteja ajipime); vazi hilo hukaguliwa kuhusu vipimo na mtindo wake kabla ya kubomolewa kwa vipande vidogo ambavyo hukatwa tena, kupimwa tena na marekebisho yoyote ya mwisho kufanywa. Bidhaa ya mwisho ni vazi la kuvutia la aina yake ambalo Ruto alivalia katika harusi ya binti yake.

"Mafundi wengi Kenya huunda mavazi kwa mashine ili wateja wajipime, lakini ninayounda hutumia vipimo vya mteja binafsi. Uundaji mavazi kwa kutumia vipimo mahsusi vya mteja ni sanaa ya kushona vazi kutoka mwanzo hadi mwisho kwa kutumia mkono," anasema Sunny, mkurugenzi wa kampuni ya Ashok Sunny Tailored Limited.

Kwa wastani kuchora mtindo asilia na kukata kitambaa huchukua muda wa hadi nusu siku, bila kukatizwa. "Yeyote anayedai kuchukua wiki moja kuunda suti akitumia vipimo mahsusi vya mteja ni tapeli. Kuanzia mwanzo hadi mwisho, koti huchukua muda wa saa 50, suruali ndefu saa 25, kisha unashona zaidi ya nyuzi 5,000 kwa mkono, kumalizia na kujipima. Angalau wiki tatu, nne kwa vazi bora," anaeleza Sunny.

ninatoza kati ya Sh60,000 na Sh250,000 kwa suti ya vipimo mahsusi," anasema.

Kwa suti zake, kitambaa daima huwa pamba, ambayo huenda ikawa kati ya 100 na 200 kwa kiwango cha ubora au sufi. "Pamba yenye kiwango cha ubora wa 100 inagharimu Sh60,000, kiwango cha 120 ni Sh100,000, ubora wa 130 ni Sh150,000 na kadhalika. Jinsi kitambaa kilivyo na ubora wa juu na kilivyo chepesi ndivyo ninavyotozwa bei ya juu. Sufi inaweza kuchanganywa na pamba na bidhaa ya mwisho itagharimu kati ya Sh250,000 hadi Sh1 milioni. Sufi ndicho kitambaa ghali zaidi duniani, na hakipatikani Kenya."

Mita moja mraba ya Sufi ni Sh600,000; suti huhitaji mita tatu. "Idadi kubwa ya wanaume Kenya huvalia suti zilizoundwa kwa polyester: ambazo zinapatikana sokoni, lakini ni nzito na si nzuri kwa mazingira yetu yenye joto. Kitambaa bora unachoweza kupata ni mseto wa polyester na pamba, ambayo ni asilimia 30 pamba. "Kwa mavazi yake yenye vipimo



Rais William Ruto wakati wa harusi ya binti yake, June na daktari raia wa Nigeria, Alexander Ezenagu, mnamo Mei 27. PICHA | MAKTABA

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media



Mtaalamu wa fashoni, Ashok Sunny, Mkurugenzi wa kampuni ya Ashok Sunny Tailored Ltd. PICHA I MAKTABA

mahsusi, Sunny husafirisha nchini kwa meli vitambaa kutoka Italia, Uingereza, Ufaransa na Ubelgiji.

Alipoanza biashara ya kuunda mavazi

**Idadi kubwa ya wanaume Kenya huvalia suti za polyester, lakini ni nzito na hazifai kwa mazingira yetu yenye joto.**

Ashok Sunny

mnamo 2013, maono yake yalikuwa ya kumvisha kila mtu. Kamwe hakuwahi kufikiri kuwa angeishia kuanzisha nembo ya uundaji mavazi ya kifahari.

Akiwa na mtaji wa Sh20,000 alizokopa kutoka kwa mama yake, Sunny, wakati huo akiwa barobaro wa miaka 22, alifungua duka dogo eneo la Umoja, Nairobi, lililokuwa na cherehani moja. Aliajiri fundi mmoja limbukeni mwenye umri wa miaka 18 naye alikuwa mbunifu wa mitindo.

Jinsi miaka ilivyosonga na akazidi kujihusisha na fasheni, kujipatia maarifa zaidi na kuimarika kifedha, alichuja orodha ya wateja wake. "Naam, nilipoanza nilishonea kila mtu. Kwa sasa, kitambaa cha kiwango cha chini zaidi cha ubora tunachotumia ni mseto wa polyester na pamba; tunataka kudumisha kiwango fulani cha ubora wa hali ya juu."

Ingawa baadhi ya watu wanaweza kumkosoa kwa hatua hiyo, Sunny anasema ni bora kwa biashara na ni ishara ya kukua kwa biashara yake. "Unapofanya biashara zaidi, uelewa na taswira yako hubadilika. Unafika mahali ambapo unaelewa vitambaa mbalimbali, viwango vyake vya ubora na mitindo mbalimbali ya ushonaji, kwa kutegemea kitambaa," anafafanua.

"Siku hizi, watu zaidi wanasafiri duniani kuliko awali. Wanajua ni aina gani inaweza KUpatikana Bangkok na gani watapata London. Lakini kwa kuwa hawawezi kusafiri kila wakati wakihitaji suti, wanataka mtu kutoka humu nchini anayeweza kutoa huduma hiyo. Nilijaza pengo hilo."

Ingawa mavazi yake huenda yakaonekana kuwa ghali sana, Sunny hakosi wateja kamwe. Anakanusha dhana kuwa suti zake ni za watu wa umri wa kuanzia miaka 40 kwenda juu, wanaojiweza kifedha. "Hiyo si kweli. Hasa, idadi kubwa ya wateja wangu ni wa miaka 30 kwenda juu hasa kutoka wafanyakazi wa ofisini, mawakili na wabunge vijana."

Anahesabu miongoni mwa wateja wake aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Upepelezi wa Jinai, George Kinoti, Mkurugenzi wa Kampuni ya Chandaria Group, Darshan Chandaria, aliye na umri wa miaka 36 na mtaalamu wa mawasiliano Mwenesi Musalia, 38.

Kwa kutaka kujua zaidi, ninamuuliza ni suti ngapi za kifahari ameunda tangu mwaka ulipoanza. "Hiyo ni data ambayo tunashughulikia kwa sasa. Sina hakika lakini kwa jumla naweza kusema suti 300. Suti za kifahari zenye vipimo mahsusi ndizo bidhaa zetu zinazonunuliwa zaidi kwa sasa," anasema Sunny kwa bashasha.

*smatiko@ke.nationmedia.com*

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*




ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni




Hadi Sakaja alipoingilia kati, polisi walikuwa wamekana uhalifu umeongezeka Nairobi

# Polisi wanapofumbia macho maovu



KWENDO
OPANGA

Inakumbukwa wazi kuwa wakazi wa Nairobi walipoelezea wasiwasi wao kuhusu kuongezeka kwa uhalifu jijini mapema mwezi jana, polisi walikanusha habari hizo.

Hasa, Kamanda wa Nairobi James Mugera alidai katika mahojiano ya moja kwa moja ya runinga kuwa ripoti za ongezeko la uhalifu zilinuiwa kuchafua jina la serikali mpya.

Mugera alidai ni visa tisa pekee vya wizi wa mabavu vilivyokuwa vimeripotiwa kati ya Septemba na Oktoba. Ni muhimu kuangalia tena kauli za Mugera.

Kwanza, aliingiza siasa katika suala hilo, akisema kilichokuwa kimebadilika sio huduma ambayo polisi wanatoa, lakini ni utawala wa kisiasa.

Hivyo basi, hofu ya wakazi wa Nairobi haikuwa na msingi wowote na ilichochewa kisiasa. Kwa kusema hivyo, ni wazi alikuwa akijaribu kutetea utawala mpya kwa kudai ulikuwa ukipakwa matope. Ni mbinu ya kijanja ambayo, kwa bahati mbaya inachafua heshima ya waathiriwa wa uhalifu kwa kuwalaumu kwa uhalifu waliotendewa. Hii ni kwa sababu, kwa kulaumu waathiriwa, wahalifu wanalindwa na kupata nguvu.

Pili, Mugera aliendeleza mtindo ambao polisi wamekuwa wakitumia na kuwa tabia yao. Umewahi kusikia polisi wakikiri kuwa uhalifu umeongezeka? Mnamo 1997 wimbi la uhalifu lilipokumba jiji la Nairobi hadi likapewa jina la Nairobbery, niliuliza mwanahabari mwenzangu kwa nini polisi walisisitiza hakukuwa na ongezeko la uhalifu. Akiwa polisi aliyeacha kazi hiyo, aliniuliza: "Unataka wakiri kuwa wanashindwa na kazi?"

Tatu, afisa huyo mkuu wa polisi alisema ni visa tisa pekee vya wizi wa mabavu vilivyokuwa vimeripotiwa ndani ya miezi miwili.

Masuala matatu yanaibuka; moja ni kuwa wizi wa mabavu ndio unaoonyesha polisi kuwa vitendo vya uhalifu vinaongezeka na, pili, kama haujaripotiwa kwa polisi, basi huwa haujatendeka. Tatu, ni Wakenya wangapi wanaopiga ripoti kuwa wamepigwa ngeta, kupokonywa mifuko au mizigo yao kunyakuliwa mikononi mwao na wezi wanaoendesha pikipiki? Kwa hakika, ni wakazi wangapi wa Nairobi wameenda katika vituo vya polisi kuripoti kuwa walisimamishwa na genge lililowaibia mali zao za thamani? Je, inamaanisha kuwa, mtu akikosa kuripoti aliibiwa simu yake huwa hajaibiwa?

Gavana wa Nairobi Johnson Sakaja alipotoa onyo kuhusu ongezeko la uhalifu baada ya rafiki yake kudungwa kisu na akakutana na Inspekta Jenerali wa polisi Japheth Koome, polisi walibadilisha kauli, mbinu na msimamo. Jamaa mwenye mamlaka, kama ambavyo Francis Imbuga angeeleza, aliingilia kati kwa niaba ya wakazi wa Nairobi.

Sakaja alisema alizungumza na Koome na wawili hao wakakubaliana kujadili suluhu ya wimbi la uhalifu. Punde, wakazi wa Nairobi walianza kuona polisi wakipiga doria katika maeneo yaliyotambuliwa kuwa hatari. Hivi ndivyo polisi wanavyofanya. Wanajitokeza kwa nguvu na baada ya siku moja au mbili, wanaondoka.

Wahalifu wanajificha au wanabadilisha vituo kwa muda huo kisha wanarudi mambo yakitulia na kuwa shwari.

Kisha akaingia Profesa Kithure Kindiki, Waziri Mpya wa Usalama wa Ndani na hivyo basi, anayeshikilia masuala ya usalama. Kama Koome, aliyetangulia, alionya wahalifu waache vitendo vyao kwa sababu "tutawasaka popote walipo."

Nimechunguza. Kila waziri na Inspekta Jenerali tangu Joseph Lenku na David Kimaiyo mtawalia mnamo 2013, anafuata mkondo huo wa kuonya, kutisha na kusikika kuwa mkali.

Wahalifu huwa wanatulia tu na kuendelea na kazi yao. Vitendo vya uhalifu havitakoma kwa sababu polisi wanaonekana wakali wakipiga doria katika ngome zao ili kuwatia hofu.

Kuzingatia ujasusi, kupenya maeneo ya wahalifu, kuwakamata, kuwashtaki na kuwafunga jela kwa miaka mingi ndiko kutamaliza na kushinda magenge ya wahalifu.

Uhalifu utapungua wakati serikali itakuwa kali kwa uhalifu na visababishi vya uhalifu na polisi kuzuia uhalifu.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "ePaper Copy"

maoni

MIKOPO YA HASLA

# Tutapata watu waaminifu kutunza Hazina hiyo?



MACHARIA
**GAITHO**

Kama Hazina ya Hasla iliyozinduliwa Novemba 30 itafanya kazi kama ilivyotangazwa, itakuwa kutimia kwa kilichoonekana kuwa ahadi ya kampeni yenye matumaini, ikiwa si ya kupotosha, na itakayompiga jeki sana Rais William Ruto ambaye kufikia sasa ameonekana kuteleza kuliko kufaulu siku za mwanzo za utawala wake.

Zaidi ya mafanikio ya kisiasa, huenda ikaleta manufaa makubwa kwa mamia ya maelfu ya wafanyabiashara wa kiwango cha chini ambao hutegemea mikopo ya kila siku au wiki kwa riba za juu kudumisha biashara zao na kutimiza mahitaji yao.

Kufikia wakati wa kuandika makala haya, maswali bado yanaulizwa kuhusu iwapo riba ya kila siku ya mikopo hiyo ni asilimia 0.002 kama ilivyotangazwa, au asilimia 0.02, lakini kwa wanaolipa riba za kufikia asilimia kumi kila siku kwa mashirika ya kukopesha kupitia simu au mitandao, huenda hayo yakawa maelezo yasiyo na maana yoyote.

Mikopo hiyo midogo itakuwa afueni kubwa kwa akina mama sokoni, wachuuzi,

wauzaji samaki, wauzaji mitumba na wafanyabiashara wengine wa kiwango cha chini ambao mahitaji yao ya kuongeza bidhaa zao kila siku, kuuza bidhaa na kulipa mikopo yao mwisho wa siku yatashughulikiwa vyema kabla ya kuanza mkondo huo siku inayofuata.

Kiwango cha mikopo hiyo, hata hivyo, kinaihitaji Hazina ya Hasla kuacha kuitwa 'Biashara Ndogo na za Kadri' jina lililobuniwa na wahusika katika idara za maendeleo na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) na badala yake kuangazia tu Biashara Ndogo. Walio na mahitaji makubwa wanaweza kutengenezewa mpango mwingine ama kutumia taasisi rasmi za kutoa mikopo.

Kwa sasa, Hazina ya Hasla itawafaa sana wafanyabiashara wadogo, lakin itawasaidia sana dhidi ya mazoea ya kuchukua mikopo ya simu inayodhibitiwa na mashirika makubwa, mengi yakiwa ushirikiano baina ya benki na kampuni za kutoa huduma za simu.

Hazina ya Hasla inafaa kushinikiza kampuni za kutoa mikopo ya simu kutathmini mienendo yake ya kuwapunja wateja, kwani kwa kiwango fulani zimeruhusiwa kukwepa baadhi ya masharti ya Benki Kuu ya Kenya kuhusu ukopeshaji, utozaji riba na utozaji faini mtu anapokosa kulipa wakati uliowekwa.

Benki, kampuni za simu na wahudumu wengine waliokuwa wamedhibiti sekta hiyo lazima sasa wapunguze riba zao ili kuzilinganisha na zile za Hasla, la sivyo wafunge biashara zao. Hata hivyo, inatarajiwa kuwa kampuni hizo zikisitisha shughuli zake, Hazina ya Hasla itapanuliwa kuziba pengo hilo.

Jambo muhimu kuelewa ni kuwa Hazina ya Hasla si pesa za bure au uporaji wa fedha za umma, bali ni hazina inayojisimamia kupitia ulipaji mikopo na inazalisha pesa zaidi za maendeleo na kuwekezwa tena. Hapo ndipo kazi inapoanza.




Wafuasi wa Kenya Kwanza wakati wa mkutano katika Uwanja wa Michezo wa Nyayo mnamo Agosti 6. Hazina ya Hasla inafaa kulazimisha watoaji mikopo kwa simu wapunguze tamaa yao ya kutoza riba za juu ambazo zinakiuka mwongozo wa Benki Kuu ya Kenya wa kutoa mikopo, kutoza riba na faini kwa wanaokosa kulipa kwa wakati uliowekwa.

**Serikali zilizopita zilikuwa na watu walioona pesa za umma kama zao, lakini utawala wa Kenya Kwanza umezidi kwa kuteua watu walioshtakiwa kwa ufisadi na makosa mengine dhidi ya Wakenya kuhudumu katika nyadhifa muhimu.**

Kampeni za mrengo wa Kenya Kwanza zilihusu utoaji pesa, ambapo raia walizikubali kwa furaha kubwa. Uhalisia uliomkumba Ruto baada ya kuchukua uongozi ulimfanya kutoa kisingizio kuwa alirithi hazina ya kitaifa ambayo pes azote ziliporwa na serikali ya Jubilee chini ya Rais Uhuru Kenyatta.

Alikosa kubaini kuwa alikuwa sehemu ya uporaji huo dhidi ya Wakenya kwa miaka kumi. Hakuna pesa za bure, kilichopo ni muundo unaotoa mikopo kwa riba za chini kwa wanaohitaji, lakini si kumtwika mzigo mlipaushuru.Swali kuu ni iwapo Hazina ya Hasla itafanya kazi kama ilivyotarajiwa, kutokana na uwezekano mkubwa wa ufisadi na usimamizi mbaya katika serikali.

Hazina ya Hasla si mkakati wa kwanza nchini Kenya uliobuniwa kusaidia na kuinua wanawake, vijana na makundi mengine yaliyotengwa. Mtu anaweza kurudi tangu utawala wa Mzee Jomo Kenyatta na kufuatilia kwa warithi wake wote, Daniel arap Moi, Mwai Kibaki na Uhuru Kenyatta, ambapo kuna mifano ya hazina za kifedha zilizobuniwa kusaidia makundi maalumu lakini zilkafungwa kutokana na uporaji.

Ni hali ya kutia hofu kuwa utawala wa Ruto ni mkusanyiko wa baadhi ya watu waliowahi kukumbwa na makosa na ambao hupuuza masuala yanayohusu uadilifu katika uongozi.

Serikali zilizopita zilikuwa na watu walioona pesa za umma kama zao, lakini utawala wa Kenya Kwanza umezidi kwa kuteua watu walioshtakiwa kwa ufisadi na makosa mengine dhidi ya Wakenya kuhudumu katika nyadhifa muhimu.

Watu kama hao wakiwa katika Baraza la Mawaziri na wengine zaidi wakitarajiwa kupewa nyadhifa mbalimbali za utumishi wa umma, inakuwa vigumu kuona kule watu waaminifu, wenye nidhamu, wazalendo watapatikana kusimamia Hazina ya Hasla.

***gaithomail@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media



Wanariadha wa Amerika Tommie Smith (katikati) na John Carlos (kulia) wakinyanyua mikono iliyovishwa glavu nyeusi kwa saluti ya 'Black Power' kupinga ubaguzi wa rangi nchini Amerika wakati wa wimbo wa taifa, baada ya kupokea medali zao za nafasi ya kwanza na ya tatu katika mbio za mita 200 za Michezo ya Olimpiki ya Mexico mnamo Oktoba 17, 1968. Kushoto ni Peter Norman wa Australia aliyemaliza katika nafasi ya pili.

■ UKWELI MCHUNGU KWA WALIO MAMLAKANI

# KIDETE KUPINGA UDHALIMU

## Kutoka Olimpiki hadi Kombe la Dunia, wachezaji wameonyesha uwezo wa kuongoza juhudi za kupinga ubaguzi wa rangi na udhalimu wa kijamii

● NA KWENDO OPANGA

Unamkumbuka Okonkwo, mhusika mkuu katika riwaya ya kwanza ya Chinua Achebe, 'Things Fall Apart' ya 1958? Alileta heshima kwa jamii yake ya Umuofia na akapanda ngazi kuwa mhusika muhimu katika masuala ya jamii hiyo kwa kuwa alikuwa mwanamieleka stadi. Ndiye aliyempokonya taji Amalinze the Cat, ambaye hakuwa ameshindwa na yeyote hapo awali.

Kutoka 1966 hadi mwanzo wa miaka ya 1970, Mkenya aliyejulikana zaidi kote duniani alikuwa polisi. Hakujulikana kwa maovu yanayotekelezwa na vikosi vya usalama. La, Kipchoge Keino alisifika kwa kuleta heshima na sifa nchini alipomshinda Mwamerika Jim Ryun katika mbio za mita 1,500 na kutwaa dhahabu katika Michezo ya Olimpiki ya Mexico.

Kutoka wakati huo, Kip, kama alivyokuja kujulikana, alidhibiti mbio hizo na mbio za masafa ya kadri kwa muda mrefu, kiasi kwamba Rais Jomo Kenyatta na mawaziri wangeangukiana wakimshangilia na kufurahia medali zake.

Katika Olimpiki hizo pia, wanariadha Tomi Smith na John Carlos wenye asili ya Amerika na Afrika, walishangaza dunia waliposhinda medali za dhahabu na shaba mtawalia katika mbio za mita 200. Timu ya taifa ya Amerika ilipocheza, waliinua ngumi zao wakiwa wamezikunja huku wamevalia glovu nyeusi.

Ilikuwa ishara ya kukataa na kupinga kudhulumiwa kwa watu weusi na harakati za kutetea haki za kiraia nchini humo. Waliporudi nyumbani, Smith na Carlos walisifiwa na kukosolewa kwa kiwango sawa. Kwa wanariadha hao, hata hivyo, Olimpiki na hiyo ilikuwa nafasi ya kuongoza dunia nzima kupinga ubaguzi wa rangi.

Mara nyingi, mashindano ya michezo duniani huwa yanapandisha hadhi ya kimataifa malalamishi dhidi ya matukio fulani, jinsi tu yanavyoonyesha umahiri na fahari ya nchi husika. Taswira hii imejitokeza katika Mechi za Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar.

Nyimbo zao za kitaifa zilipokuwa zikichezwa, wachezaji wa timu ya Iran walinyamaza. Kimya chao kilishangaza dunia nzima. Kwenye picha waliyopigwa kabla ya mechi yao, wenzao kutoka Ujerumani walifunga midomo yao kwa mikono, jambo lililozungumziwa na wengi duniani.

Timu mbili kutoka mabara tofauti yenye tamaduni tofauti, zilizocheza siku tofauti na katika viwanja tofauti, zilikuwa zikilalamika: Wairan kuhusu msako unaoendeshwa na serikali yao dhidi ya watetezi wa haki za binadamu za wanawake na Wajerumani kuhusu Fifa kwa kuwanyima uhuru wa kuelezea hisia zao kuunga mkono jamii za mashoga (LGBTQ). Kuna sababu: ushoga ni marufuku nchini Qatar.

Mtetezi wa haki za mashoga kutoka Uingereza, Peter Tatchell, alikuwa amelalamikia suala hilo katika miji ya London na Doha siku chache kabla ya michezo hiyo kuanza. Alilalamikia hatua ya Qatar kukiuka haki za mashoga, wanawake na wafanyakazi wahamiaji. Alitaka kuwaunga mkono watetezi wa haki Qatar ambao hawangetoa sauti zao kwa kuogopa kukabiliwa na serikali yao.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

# Nguvu za michezo katika kutetea haki



Wachezaji wa Iran wakisikiliza wimbo wa taifa kabla ya mechi yao ya Kundi D ya Kombe la Dunia Qatar 2022 dhidi ya Uingereza katika Uwanja wa Kimataifa wa Michezo wa Khalifa, jijini Doha, mnamo Novemba 21.

Usiku wa kuamkia michezo hiyo, Rais wa Fifa, Gianni Infantino, alilaumiwa na kukosolewa kote duniani kufuatia kikao alichofanya na wanahabari kilichodumu saa moja na nusu. Alitetea Qatar dhidi ya madai ya ukiukaji wa haki za binadamu, ubaguzi dhidi ya mashoga, mauaji na mishahara duni, hasa kwa wafanyakazi wahamiaji, wengi wao wakishiriki ujenzi wa viwanja na miundomsingi inayotumika kuendesha Kombe la Dunia.

"Leo nahisi kuwa raia wa Qatar. Leo nahisi kuwa Mwarabu. Leo nahisi kuwa Mwafrika. Leo nahisi kuwa mlemavu. Leo nahisi kama mfanyakazi mhamiaji," akasema. Lakini kwa nini? "Bila shaka mimi si raia wa Qatar, si Mwarabu, si Mwafrika, si shoga, si mlemavu. Lakini nahisi kuwa hayo kwa sababu ninajua mtu anavyohisi kwa kubaguliwa, kudhulumiwa kama mgeni katika nchi ya kigeni."

Alilenga kuelekeza mtazamo wa dunia katika kandanda wala si siasa zinazohusu vitendo vya Qatar katika ukiukaji wa haki za binadamu na vifo vya wafanyakazi wahamiaji. Alijipaka tope la kisiasa alipolaumu nchi za Magharibi kwa kuendesha dhuluma kwa zaidi ya miaka 3,000, hasa jinsi zilivyoshughulikWaWaia wahamiaji na jamii ndogo.

Alionekana kuzua mtafaruku baina ya Magharibi na maeneo mengine kudhihirisha kuwa kandanda na siasa zina uhusiano wa karibu: "Tunafunzwa mafunzo mengi kutoka kwa Wazungu, kutoka nchi za Magharibi ... Kile Wazungu wamekuwa wakifanya kwa miaka 3,000 iliyopita, tunapaswa kuwa tukiomba msamaha kwa miaka 3,000 ijayo kabla ya kuanza kutoa mafunzo."

Kandanda huwaleta watu pamoja, na Kombe la Dunia la Fifa huleta dunia katika nchi mwenyeji kwa njia ya kawaida na ya vyombo vya habari. Vyombo vya habari vinapeleka dunia kwa Kombe hilo na kupeleka Kombe la Dunia la Fifa kwa dunia.

Shirika la habari la Associated Press lilisimulia hadithi ya mwanamke raia wa Iran anayeishi kusini mwa Uhispania, aliyesafiri hadi Qatar siku ambayo Iran ilikuwa ikicheza mechi yake ya pili na kushinda. Aliambia shirika hilo kuwa hakufurahia ushindi huo kwa kuwa haukuwa muhimu. Lengo lake kuu lilikuwa kulalamika dhidi ya ukatili wa Iran dhidi ya wanawake. Alikuwa mwandamanaji wala si shabiki au mtu aliyekuwa akitafuta furaha.

Wakati wa mechi ya kwanza ya timu hiyo, waandamanaji walisherehekea sana. Hata hivyo, wakati wa mechi ya pili, wafuasi wanaounga mkono serikali walikusanywa na kufika kwa idadi kubwa kuwatisha na kuwaondoa waandamanaji, kuwapiga picha na kupinga kauli zao na zile za kusifu Iran na kuwasifu maafisa wa Qatar kwa kuwanyang'anya mabango ya kuikosoa serikali ya Iran.

Je, mwandishi George Orwell angetambua Kombe la Dunia nchini Qatar? Alifananisha michezo ya kimataifa na "mwigo wa vita." Haya ndiyo aliyoandika Desemba 1945 kuhusu michezo hiyo: "Michezo yenye uzito huwa haizingatii usawa. Huwa inaandamwa na chuki, wivu, kiburi, ukiukaji wa sheria zilizowekwa na furaha katika kushuhudia ghasia: kwa njia nyingine, ni vita bila ufyatulianaji risasi."

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*



Wachezaji wa Ujerumani wafumba vinywa vyao kabla ya mechi yao ya Kundi E ya Kombe la Dunia Qatar 2022 dhidi ya Japan katika Uwanja wa Kimataifa wa Michezo wa Khalifa jijini Doha, mnamo Novemba 23.

**Leo najihisi Mqatari. Najihisi Mwarabu. Najihisi Mwafrika. Leo najihisi shoga. Leo najihisi mlemavu. Leo najihisi mfanyakazi mhamiaji:Najua maana ya kubaguliwa, kama mgeni katika nchi ya kigeni**

Rais wa Fifa Gianni Infantino

Nation Media Group "ePaper Copy"

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# Chombo cha Nasa chavunja rekodi ya dunia



Chombo Orion cha Shirika la Amerika la Usafiri wa Angani (NASA) kimefikia kiwango muhimu kwenye safari yake ya kuzunguka Mwezi.

Mnamo Jumatatu, chombo hicho kilikuwa kimesafiri umbali wa kilomita 430,000 kutoka Duniani - umbali mrefu zaidi ambao chombo kilichotengenezwa kubeba mwanadamu kimewahi kusafiri. Chombo hicho hakina abiria wakati huu lakini kikikamilisha safari yake bila tatizo lolote kingine kitakachorushwa angani kitakuwa na wanaanga. Chombo hicho kimepangiwa kurushwa miaka miwili ijayo.

Nasa inapanga ziara angani kwa kutumia Orion. Safari hizo ni sehemu ya mpango wa Artemis, unaolenga kurudisha binadamu mwezini baada ya miaka 50. Hatua ya Jumatatu inaashiria nusu ya umbali wa safari hiyo. "Hatua hiyo inatufunza kuhesabu idadi ya siku zetu ili kuweze kuelewa zaidi," akasema Mike Sarafin, meneja wa mpango wa Artemis..

"Kiwango hicho kinatupa nafasi kutathmini mapungufu yaliyopo, kuelewa mwendo wake na kubaini tutakayoimarisha kwenye safari ijayo kwani itahusu kuwepo kwa binadamu kwenye chombo."

Chombo hicho kilirushwa angani kutoka Kituo cha Anga cha Kennedy, Florida, Novemba 16. Safari yake itachukua siku 26. Safari hiyo ni jaribio la kuhakikisha chombo kitakachorushwa tena kitakuwa salama kubeba wanaanga. Chombo hicho kinasaidiwa kusafiri angani na huduma maalumu inayotolewa na Mamlaka ya Usafiri Angani ya Ulaya (ESA).

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# MAJARIBIO YA INJINI YA HAIDROJENI KWA NDEGE




Injini ya Rolls Royce Trent XWB katika kiwanda jijini Derby, Uingereza. Faida ya haidrojeni ikilinganishwa na betri ni kuwa inatoa nguvu za kwa kilo.

LONDON

Katika eneo la kijeshi kwenye Nyika ya Salisbury nchini Uingereza, injini ya ndege ndogo inafanyiwa majaribio ambayo huenda siku moja yakaleta mageuzi makubwa katika sekta ya usafiri wa ndege.

Ni injini inayokaribiana na zile za kawaida. Ni aina ya Rolls-Royce AE-2100A, muundo unaotumika sana katika ndege kote duniani. Kilicho tofauti kuihusu ni aina ya mafuta yanayotumika. Hii ni mara ya kwanza ambapo injini ya ndege ya kisasa itatumia gesi ya haidrojeni.

Kando na muundo wake unaojumuisha nyaya na mifereji mingi, imewekwa vizuri katika eneo inakofanyiwa majaribio. Wahandisi wamezunguka viwambo kadhaa katika chumba cha kuidhibiti, mbali kiasi kutoka ilipo.

Majaribio hayo yanafanywa na kampuni ya Rolls-Royce, baada ya kufanyiwa ukarabati maalumu mjini Derby kwa ushirikiano na shirika la ndege la easyJet. Lengo la haraka ni rahisi - kuonyesha inawezekana kuendesha na kudhibiti injini ya ndege kwa kutumia gesi ya haidrojeni, badala ya mafuta yanayotumika na ndege za kawaida.

Mpango wa siku za usoni ni kuhakikisha gesi ya haidrojeni inatumika zaidi katika kupanua sekta ya uchukuzi wa ndege na kupunguza gesi hatari zinazosababisha mabadiliko ya hali ya hewa."Sababu ya kulenga kuanza kutumia haidrojeni ni kupunguza utoaji wa gesi

zinazoharibu hewa," anaeleza Alan Newby, mkurugenzi wa teknolojia ya uchukuzi wa ndege katika Rolls-Royce. "Kwa kawaida, tungeendesha injini hii kwa mafuta ya taa. Mafuta ya taa ni haidrokaboni hivyo hutoa gesi ya kaboni dioksidi yakichomeka. "Uzuri wa kuangalia mafuta kama haidrojeni ni kuwa huyana wa kaboni, hivyo yakichomeka hayatoi gesi ya CO2."

Mradi huo unafadhiliwa na shirika la easyJet ambalo lilitoa pauni milioni kadhaa kugharamia majaribio ya mwanzo. Shirika hilo linaamini kawi ya haidrojeni ndiyo njia bora zaidi ya kupunguza utoaji wa gesi hatari kutoka kwa ndege. "Tulianza miaka michache iliyopita kutathmini tunachoweza kutumia kama mafuta ya ndege siku za usoni," akasema Afisa Mkuu wa Uchukuzi wa easyJet, Davis Morgan.

"Tuliangalia teknolojia ya betri yake, na ilikuwa dhahiri kuwa teknolojia hiyo haingefaulu kimatumizi kwa ndege kubwa za uchukuzi ambazo tunatumia.

"Tumeamua kuwa haidrojeni ni pendekezo zuri sana kwetu."

Manufaa ya haidrojeni ikilinganishwa na betri ni kuwa inatoa kawi nyingi sana kwa kilo. Betri ni nzito sana kuendesha ndege kubwa. Hata hivyo, itachukua muda mrefu haidrojeni kuanza kutumika katika uchukuzi wa ndege. Majaribio yaliyofanyika kufikia sasa yanaonyesha injini ya ndege inayotumia haidrojeni inaweza kuanzishwa na kuendeshwa kwa kasi ya chini.

Hata hivyo, utafiti na uwekezaji Zaidi utahitajika kufikia kiwango cha ujenzi wa injini mpya inayoweza kuendesha salama ndege ya abiria.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya afrika

■ KUNA MAGAIDI WAPATAO 8,000 KOTE NCHINI

# VITA VIKALI DHIDI YA AL-SHABAAB SOMALIA

• MOGADISHU

Serikali ya Somalia imetangaza "vita vikali" dhidi ya kundi la kigaidi la Al-Shabaab na imekubali kutumia mbinu kadhaa katika juhudi za kukabiliana na ugaidi – ambazo, licha ya baadhi yake kutajwa mapema na vyombo vya habari kuwa ufanisi wa kijeshi – zinaonekana kuwa ndefu na ngumu.

Kundi hilo mwanachama wa Al-Qaeda lilifurushwa kutoka miji mikubwa ya Somalia miongo kadhaa iliyopita lakini linathibiti sehemu kubwa ya maeneo ya mashambani ya nchi ambako makundi yenye silaha yaliungana dhidi ya wapiganaji hao miaka ya hivi majuzi.

Koo mbili eneo la kati ya Somalia linalokumbwa na ukame, kwa kuchoka kuishi chini ya utawala wa Al-Shabaab, zilianza uasi dhidi ya kundi hilo mnamo Julai na umeenea kwa haraka katika maeneo ya Hirshabelle na Galmudug.

Mnamo Septemba, Jeshi la Kitaifa la Somalia na makamanda waliopata mafunzo Amerika walijiunga na mzozo huo wakisaidia wapiganaji wa koo wanaoitwa "macawisley" kutokana na mavazi ya kitamaduni wanayovalia.

"Serikali inataka kutumia juhudi za sasa na kuhimiza aina hiyo ya maasi kote katika maeneo yanayothibitiwa na Al-Shabaab Somalia," akasema Omar

...Endelea Uk 26



Mwanajeshi wa kike wa Jeshi la Kitaifa la Somalia, Nimo Ibrahim, alipokuwa akihojiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kismayu mnamo Januari 21, 2014. PICHA | EVANS HABIL

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Mogadishu yaapa kuzima magaidi

Kutoka Uk 25

Mahmood, mtafiti katika International Crisis Group.

Ingawa haijafahamika ni wapiganaji wangapi wanaohusika katika makabiliano ya sasa, vita hivyo vimechacha na kufikia kiwango ambacho hakijawahi kuonekana kwa miaka mingi, huku ripoti ambazo hazijathibitishwa zikisema mamia wameuawa katika mapigano. Duru nchini Somalia zinaashiria kuwa vita hivyo huenda vinahusisha "macawisley" kati ya 2,000 na 3,000. Inaaminika kuwa kuna magaidi kati ya 5,000 na 8,000 kote nchini humo.

Kwa kusaidiwa na mashambulizi ya droni za Amerika na vifaa vya kijeshi kutoka Kikosi cha Mpito cha Muungano wa Afrika, juhudi hizi za pamoja zimefukuza Al-Shabaab kutoka mikoa muhimu ya Hiran na Middle Shabelle.

Mnamo Julai, rais mpya aliyechaguliwa nchini humo Hassan Sheikh Mohamud alitangaza mpango wa serikali yake kuhusiana na magaidi hao wa Kiislamu: kuwapiga kijeshi, kukata njia za kupata pesa na kukabiliana na mafunzo yao makali. "Sera za awali zilikuwa za kijeshi… kushambulia, kuharibu. Lakini shida ya Shabaab ni zaidi ya kijeshi," akasema.

Kama hatua ya kwanza, alimteua Mukhtar Robow - mmoja wa waanzilishi wa Al-Shabaab aliyeacha kundi hilo mnamo 2017 - kuwa waziri wa masuala ya kidini kupinga mafunzo ya Kiislamu yenye itikadi kali ya kundi hilo.

Mnamo Oktoba, serikali ilitishia kubatilisha leseni za biashara za wafanyabiashara walioilipa "ushuru" kwa Al-Shabaab na kuchangia mamilioni wanayopata kupitia vitisho. Mshirika mkuu wa kigeni wa Somalia, Amerika, imetangaza zawadi ya dola 10 milioni (Sh1.2 bilioni) kwa habari zitakazovuruga ufadhili wa Al-Shabaab.

Mwaka huu, Amerika ilituma wanajeshi wake tena Somalia, na kubadilisha uamuzi uliokuwa chini ya utawala wa aliyekuwa rais Donald Trump. "Serikali inaendelea kujaribu na kujenga imani miongoni mwa umma ili waweze kukataa kundi hili. Bado hatujapima ufanisi wa maamuzi hayo," akasema Samira Gaid wa taasisi ya Hiraal Institute, kundi la wataalamu wa usalama lenye makao yake Somalia.

Huenda magaidi hao wakawa wamepoteza eneo wanalothibiti lakini wanaendelea kupigana, akasema Mahmood. "Hata wakishindwa sasa, watatafuta njia za kuhujumu serikali ili waweze kurudi." Magaidi hao wamerudi katika baadhi ya maeneo waliyoondoka kufuatia mapigano na kuzidisha mashambulizi kwa mabomu.

Mnamo Oktoba 29, Somalia ilishuhudia shambulizi baya zaidi tangu 2017, mabomu mawili yalipolipuka ndani ya gari jijini Mogadishu na kuua watu 121 na wengine 333 kujeruhiwa.

Gaid alisema uasi wa koo ni "tisho kubwa" kwa Al-Shabaab na magaidi hao wanajiandaa kuukabili. "Wanajitahidi sana kuzima uasi huo na kushawishi koo zingine dhidi ya kujiunga na vita," akasema.

Rais Mohamud aliambia wabunge mnamo Novemba kuwa "hakuna kurudi nyuma wala kushindwaa". Lakini kukomboa eneo ni nusu tu ya lengo. "Sehemu ngumu zaidi ni kuendelea kudhibiti eneo hilo" na kuhakikisha watu wanaweza kupata huduma ili waone manufaa ya utawala wa serikali, akaongeza.

Ufanisi wa awali dhidi ya magaidi hao umepotea kutoikana na uhasama mkali wa koo, ambao Al-Shabaab hutumia kupata nguvu. Ghasia za koo tayari zimeripotiwa katika baadhi ya maeneo yaliyokombolewa majuzi kutoka kwa magaidi hao. Mohamud alisema serikali inaonekana kutaka kupanua operesheni yake, lakini kufanya hivyo kunaweza kuwa kazi ngumu.

Haijabainika iwapo koo zinaweza kuungana dhidi ya Al-Shabaab kusini mwa Somalia, ambako magaidi wangali na ushawishi. Al-Shabaab wamehimili vita vya kijeshi kwa miaka 15 na Mohamud mwenyewe alitangaza Julai kuwa "kuna sababu nzuri" za kuzungumza na magaidi hao. "Lakini sasa hatuko katika hali ya kuzungumza na Al-Shabaab," akasema. "Tutafanya hivyo wakati unaofaa. Tutajadiliana nao."

Akasema Gaid: "Imekuwa wazi kwa serikali kuwa mazungumzo au maridhiano yanaweza kufanyika ikiwa na usemi zaidi." Vita hivi "vitasaidia kupatia serikali usemi mkubwa wa kushiriki mazungumzo baadaye".

Wakati huo huo, vikosi vya usalama vya Somalia vilizima shambulizi la Al-Shabaab la saa kadhaa katika mkahawa maarufu jijini Mogadishu ambao waliteka usiku kucha na kuua raia wanane mnamo Jumatatu.

Shambulizi hilo lilianza saa moja usiku Jumapili kwa ufyatuliaji mkali wa risasi na milipuko magaidi walipoteka mkahawa wa Villa Rose, unaotembelewa kwa wingi na wabunge na maafisa wengine wa serikali.

Karibu saa 21 baada ya shambulio kuanza, Sadik Dudishe, msemaji wa polisi wa taifa, aliambia wanahabari "operesheni ya kusafisha Villa Rose imeisha". Magaidi waliua raia wanane waliokuwa wakiishi katika mkahawa huo na maafisa wa usalama wakafaulu kuokoa raia wapatao 60, hakuna raia aliyejeruhiwa", akaongeza. Afisa mmoja wa usalama pia aliuawa katika operesheni hiyo, akasema.

Mkahawa wa Villa Rose unapatikana katika eneo "salama" katikati mwa jiji, hatua chache kutoka ofisi ya Rais wa Somalia Hassan Sheikh Mohamud, hali inayozua maswali kuhusu jinsi magaidi hao waliweza kukwepa vizuizi vingi katika eneo hilo.

Al-Shabaab, kundi ambalo limekuwa likijaribu kupindua serikali ya Somalia kwa miaka 15, lilikiri kutekeleza shambulizi hilo. Kundi hilo limezidisha mashambulizi dhidi ya raia na wanajeshi huku serikali iliyochaguliwa majuzi ya Somalia ikiendeleza sera ya "vita vikali" dhidi ya magaidi hao wa Kiislamu.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*



Wanajeshi wa Somalia wakikagua eneo la mlipuko wa bomu lililotegwa ndani ya gari mjini Mogadishu mnamo Oktoba 15, 2017.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya dunia

■ HAKEEM JEFFRIES AWEKA HISTORIA KATIKA SIASA ZA AMERIKA

# ‘OBAMA WA BROOKLYN’



Hakeem Jeffries (New York) akihutubia wanahabari baada ya kuchaguliwa kiongozi wa Bunge la 118 na kundi la wabunge wa chama cha Democratic jijini Washington, DC mnamo Novemba 30. Jeffries alichaguliwa kumrithi Spika Nancy Pelosi kama kiongozi wa chama cha Democratic katika bunge hilo mwaka ujao, na kumfanya mtu wa kwanza Mweusi kuongoza kimoja cha vyama vikuu katika bunge hilo.

## Kupanda kwa mbunge wa New York hadi kileleni mwa Chama cha Democratic baada ya kuondoka kwa Pelosi kunamfanya mtu wa kwanza Mweusi kuongoza chama kikuu katika Bunge la Amerika

• WASHINGTON

Mbunge Hakeem Jeffries wa Amerika wiki hii alichaguliwa kumrithi Nancy Pelosi kama kiongozi wa chama cha Democratic katika Bunge la Wawakilishi, Amerika.

Mbunge huyo wa New York, mwenye umri wa miaka 52, ambaye amehudumu kwa mihula minne, ameshikilia cheo cha tano chenye hadhi ya juu katika uongozi wa Democratic tangu 2019.

Kupanda kwake hadi nafasi ya juu, iliyoshikiliwa na Pelosi kwa miongo miwili, kunamfanya mtu wa kwanza mweusi kuongoza chama kikuu nchini Amerika.

Lakini atakuwa kiongozi wa wachache, sio spika. Katika uchaguzi wa katikati ya muhula mwezi jana, wanachama wa Republican hawakupata ushindi mkubwa jinsi wengi walivyobashiri, lakini walipata udhibiti mdogo katika Bunge hilo.

Mwanachama wa Republican, Kevin McCatharthy, kutoka California, anayehudumu sasa kama kiongozi wa wachache, aliteuliwa na chama kuwania kiti cha spika wa Bunge hilo. Lakini ni lazima apate kura nyingi kutoka kwa Bunge lote – kura 218 - Januari ndipo apate wadhifa huo.

Pelosi, 82, alipotangaza kustaafu kwake Novemba 17, alisema: “Wakati umefika kwa kizazi kipya kuongoza wabunge wa chama cha Democratic.”

Inaonekana hatua hiyo ilishirikisha manaibu wawili wa Pelosi - Stany Hoyer, 83, na Jim Clyburn, 82 - ambaa walitoa taarifa haraka kuhusu mipango yao ya siku zijazo. Wawili hao walimwidhinisha Jeffries, huku Clyburn akiandika kuwa lengo lake ni kufanya kila awezalo “kusaidia kizazi kipya cha viongozi wa chama cha Democratic ambao natatumai watakuwa Hakeem Jeffries, Katherine Clark na Pete Aguilar.”

Kwenye barua kwa wenzake katika chama, Jeffries alikuwa ameomba wajumbe hao wa Democratic wamuunge mkono “huku kwa mara nyingine tuki-

Endelea Uk 28

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Mweusi wa kwanza kuongoza chama kikuu US

Kutoka Uk 27

jiandaa kwa wakati muhimu." Wakati huo, alimpongeza Pelosi akimtaja kuwa "Spika mzuri zaidi katika historia ya Amerika". "Ni mikono thabiti ya kutegemewa nyakati ngumu ambazo zimekabili taifa letu," akaongeza.

Kwenye uchaguzi wa faragha wa uongozi uliofanywa wiki hii, mbunge wa kike Katherine Clark, 59, wa Massechusetts alishinda wadhifa wa kiranja, kiti cha pili kwa hadhi katika uongozi wa Democratic. Naye Pete Aguilar, 43, wa California, ambaye wakati huu ni naibu mwenyekiti wa kundi la wabunge wa Democratic, alichaguliwa kumrithi Jeffries katika wadhifa wa mwenyekiti.

Mabadiliko hayo katika uongozi yatachangia kuzima malalamishi kutoka kwa baadhi ya wapigakura wa Democratic kuwa viongozi wa chama chao ni wazee zaidi.

Lakini viongozi hao wapya watatu, wenye umri mdogo, wanaonekana kuegemea zaidi mrengo wa viongozi wa zamani wa chama hicho. Jeffries mwenyewe mara kadhaa amekosana na mrengo wa kushoto wa chama hicho cha Democratic.

Ni wakili aliyezaliwa na kulelewa katika wilaya ya Brooklyn, New York. Alihudumu katika Bunge la jimbo la New York kabla ya kuwania kiti cha Bunge la Wawakilishi mnamo 2013. Ujumbe wake ulikuwa mwepesi: "Washington imevunjika. Bunge la Congress halifanyi kazi. Watu wanateseka. Tunahitaji mengi zaidi."

Wakati wa kampeni, alilinganishwa na "Barack Obama wa Brooklyn", mlinganisho ambao alikataa kwani hakuona mfanano wowote kitalaamu kati yake na rais huyo wa zamani. Tangu alipoingia ofisini, amejijengea sifa kama mbunge mbishani, mwenye ushawishi miongoni mwa wenzake huku uwezo wake ukiimarika. Kama kiranja wa kundi la Wabunge Weusi, aliongoza wenzake kulalamika vikali bungeni 2015 kufuatia msururu wa mauaji ya Waamerika Weusi na polisi.

Wakati fulani alitoa heshima zake bungeni kwa mwanamuziki wa mtindo wa Rap, The Notorious B.I.G. Mwanamuziki huyo alipewa jina Christopher Wallace, alipozaliwa katika wilaya anakotoka Bw Jeffries. Aliuawa kwa kupigwa risasi mnamo 1997.

Wakati wa maadhimisho ya miaka 20 tangu kifo chake, Jeffries alisema msanii huyo aliwakilisha "Ndoto halisi ya Amerika" huku akikariri baadhi ya maneno katika kibao chake cha, "Juicy" alichokitoa 1994.

Wakati wa urais wa Trump, Jeffries mara kwa mara alishutumu wanachama sugu wa chama cha Republican ambao walikuwa wakiunga mkono sera mbovu za kiongozi huyo bila kuzikosoa.

Mnamo 2020, alihudumu kama mmoja wa wasimamizi saba wa Democratic wakati wa mchakato wa kusikizwa kwa kesi ya kwanza ya kumng'oa mamlakani Rais Donald Trump.



Spika wa Bunge la Wawakilishi Amerika anayeondoka Nancy Pelosi (kushoto), mfuasi wa chama cha Democratic California akizungumza na Mbunge Hakeem Jeffries, mfuasi wa Democratic New York, baada ya kuhutubia Bunge jijini Washington, DC, Novemba 17.

Aidha, Jeffries ameonya kuwa McCarthy---ambaye kiongozi wa wabunge wa Republican ni "mradi wa Donald Trump."

Huku Democratic kikidumisha mamlaka katika chumba cha juu cha Congress, kiongozi wa wengi katika Seneti Chuck Schumer atasalia katika cheo chake. Hii ina maana kuwa viongozi wa Democratic katika majumba mawili ya Congress watatoka katika jimbo la New York.

*** *** ***

Bila shaka kuna mabadiliko ya kizazi yanayoshuhudiwa katika ngazi za juu za uongozi wa chama cha Democratic. Wanaondoka Pelosi, 82, na Hoyer, 83, ambao waliongoza kundi la wabunge wa chama hicho kwa karibu miaka 20.

Jeffries, ambaye ni mdogo wao kwa miaka 30 amechaguliwa kwa urahisi kumrithi Pelosi, kwani hakukabiliwa na upinzani mkali. Pia aliungwa mkono na viongozi wanaoondoka.

Jeffries ni Mwamerika Mweusi wa kwanza kushikilia wadhifa mkubwa kiasi hicho katika Congress. Na kufuatia kuteuliwa kwa Wawakilishi Clark na Aguilar katika ngazi mbili za uongozi zinazofuatia, kwa mara ya kwanza katika historia ya Congress uongozi wa Democratic hautakuwa na watu weupe.

Hayo ni maendeleo makubwa katika bunge hilo. Lakini kabla ya kila mtu kujisahau na kusherehekea mabadiliko hayo, ni bora kuuliza iwapo mtindo wa chama hicho kuendesha masuala yake utakuwa tofauti ndani ya miaka miwili kikiwa upande wa walio wachache.

Tathmini ya haraka ya wasifu wa Jeffries inaonyesha amekuwa na safari mrefu kisiasa: kwanza ni wakili, kisha alihudumu katika ikulu ya New York na baadaye akajiunga na Congress. Ingawa ni mwenyekiti wa kundi la Congressional Progressive Caucus (CPC), wengine katika mrengo wa kushoto tayari wamemtaja kuwa "kiongozi mwingine wa Democratic".

Na licha ya Jeffries kusisitiza kuwa yeye ni "kiongozi Mweusi mwendelevu katika Democratic" pia aliwahi kusema: "Wakati hautafiki ambapo nitaunga mkono ujamaa wa mrengo wa kushoto katika chama cha Democratic".

***- BBC***

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya dunia

■ UTAPELI KATIKA USAFIRI WA KIDIJITALI

# MATAPELI WA LIKIZO WAENEA

## Mitandao ya kijamii inashawishi watu kuonja maisha ya likizo za kifahari, lakini inakuwaje mambo yakiharibika?

● RIO DE JANEIRO



Visa vya utapeli vinavyohusu usafiri kidijitali vinazidi kuwa tatizo "sugu duniani" kulingana na Shirika la Utalii Duniani (UNWTO), tawi la Umoja wa Mataifa.

Mamia ya wanawake raia wa Brazil wamegundua hili kwa uchungu mwingi, baada ya kulipia likizo za kifahari kupitia mwanamume ambaye akaunti yake ya Instagram hung'aa kwa hoteli za kifahari ugenini.

Desemba iliyopita, *Maria aliamua kwenda likizo mbali na joto la msimu wa kiangazi nchini Australia na kupeleka familia yake kwa likizo ya kuteleza kwenye barafu Ulaya. Ilikuwa ziara yake ya kwanza tangu janga la Covid na alitaka iwe ya kipekee. Hivyo alilipa dola za Amerika 20,000 (karibu Sh2.4 milioni) kwa wakala wa usafiri, Rafael Bessa, raia mwenzake wa Brazil aliyependekezwa na rafiki na akafunga safari ndefu kuelekea kaskazini.

Mwanzoni, kila kitu kilikuwa shwari, lakini Maria alipokuwa akiondoka kwenye hoteli ya tatu, meneja alimwambia chumba chake hakikuwa kimelipiwa.

Matukio mengine mawili ya kushtua yalifuatana mfululizo. Maria alipowasiliana na Rafael Bessa kuomba usaidizi, aligundua hakuweza kuzungumza na msimamizi wa hoteli kwa Kifaransa, licha ya madai yake kuwa alisomea shule ya kifahari ya bweni katika milima ya Alps. Kisha, familia hiyo ilipoabiri gari la moshi kuelekea kituo chao kilichofuata, kulikuwa na tatizo na tiketi: alikuwa amewapa tiketi mbili zenye nambari sawa, kumaanisha ni moja pekee iliyokuwa halali.

Katika hoteli, tukio sawa lilizuka: Maria alilazimika kulipia bili, ingawa alikuwa amelipia kila kitu. Mwanzoni alidhani Rafael Bessa hakuelewa kazi hiyo. "Kisha nikasema, la, hili si kosa, hii ni maksudi. Hii ni kwa nia mbaya."

Kwa jumla, Maria anasema alipoteza dola za Amerika 30,000 (karibu Sh3.6 milioni) katika likizo hiyo – dola 15,000 (karibu Sh1.8 milioni) alizolipa kabla ya likizo zikiongezwa dola 15,000 (karibu Sh1.8 milioni) za ziada alizolipa katika hoteli moja tu. Maria anasema licha ya kumweleza kuwa alikuwa amelipia chumba, Rafael Bessa alisema alikuwa amemhifadhia huduma za ziada bila malipo - lakini hakuwa amefanya hivyo, na hoteli ikamlipisha bei kamili ya kiasi cha juu sana kwa chumba hicho maalumu. Ahadi za Rafael Bessa za kurudisha pesa hizo ziliishia kuwa hewa, akasema Maria.

Ingawa alimtumia "thibitisho" mbalimbali za kutuma hela, pesa hizo hazikuwahi kuingia katika akaunti yake.

Aliposimulia masaibu yake kwenye mtandao wa kijamii, anasema wakili wa wa Rafael Bessa aliwasiliana naye, akiahidi kumrudishia dola 20,000 bora tu atie sahihi mkataba wa kutozungumzia suala hilo. Alikataa. Tulimtaka Rafael Bessa kutoa maoni kuhusu madai ya Maria. Alisema kuwa kulikuwa na "tatizo" ambalo hakufafanua kuhusu bei ya moja ya hoteli hizo, na kuwa chumba katika bei hiyo hakikuwa kimejumuishwa. Alituma pia nakala za tiketi za treni - ambazo Maria alisema zilikuwa na nambari sawa za ununuzi.

Mwanamke mwingine raia wa Brazil, Ana Jalenna, alilipia ziara ya kuteleza kwenye barafu kwenye milima ya Alps na pia likizo ya msimu wa kiangazi nchini Italia kupitia Rafael Bessa, baada ya kumwandalia likizo "ya ajabu" ya familia yake Brazil.

Alilipa nusu ya bili kwa pesa tasilimu na walikuwa wamekubaliana kuwa atalipa zilizobakia kwa kutumia kadi. Baadaye muda, alishangaa kuona malipo kwa Shirika la Ndege la Uingereza yakijitokeza kwenye akaunti ya kadi yake na akampigia simu kumuuliza.

Yalikuwa malipo ya chumba cha hoteli nchini Italia, akamwambia. Kwa kutoamini, alitumia hoteli hiyo baruameme na akaambiwa hakuna malipo yaliyokuwa yamefanywa.

Ana aliamua kumwitisha Bessa thibitisho kuwa angalau alikuwa amelipia hoteli katika kituo cha barafu. Alimpa nambari za vyumba viwili, lakini hoteli ikamwambia zilikuwa feki. "Nilipoteza hela, ndoto, ziara. Nilipoteza kila kitu," anasema. Jambo hilo limejirudia tena na tena. Wateja wanafika katika vituo vyao vya likizo, wanapata hoteli haijalipiwa, na wanashindwa kumpata Bessa awarudishie pesa zao. Bessa alikanusha madai ya wateja wake, akisema "ameshtuka." "Nimeshangazwa sana na kiwango cha makosa; asilimia 90 ya ukweli wenu ni uongo," akaandika.

Shirika la Utalii Duniani (UNWTO) linasema mitandao ya kijamii inazidi kutumiwa na mawakala wa usafiri kshawishi wateja kununua likizo wanayotamani - ambayo wao pia wanaweza kuchapisha mitandaoni.

"Kwa sababu zinatangazwa katika mitandao ya kijamii, watalii wanaweza kudhani huduma hizi ni za kutegemewa zaidi kushinda ambazo wangepata kwenye tovuti za kawaida," anasema afisa anayesimamia masuala ya kisheria katika UNWTO Alicia Gomez.

Wakati huo huo, visa vya utapeli kuhusu usafiri kidijitali vimepanda kote duniani, anasema Gomez. "Suala hilo limekuwa tatizo sugu duniani. Wateja wengi nchini na serikali zinaripoti kuongezeka kwa utapeli mitandaoni, na idadi hiyo huenda ikawa hata ya juu zaidi kwa sababu watalii wengi wanaolaghaiwa hawapigi ripoti kutokana na aibu na majuto."

Shirika hilo limebuni mfumo maalumu wa kulinda watalii ambao hufafanua majukumu ya kampuni za mitandao ya kijamii, serikali na wateja na kuelezea jinsi mashirika ya umma na ya kibinafsi yanavyoweza kufanya kazi pamoja kwa njia bora.

Mataifa saba yamejiunga na mfumo huo kufikia sasa, na kuufanya sehemu ya sheria zake za kitaifa, huku nchi nyingine ikiwemo Brazil, zikiwa kwenye mchakato wa kufanya hivyo.

Meta, kampuni inayomiliki Instagram na Facebook, ilisema: "Haturuhusu vitendo vya utapeli katika mitandao yetu na tunashirikiana na maafisa wa usalama kufanya uchunguzi na kuwang'oa matapeli. "Tunaendelea kuwekeza katika teknolojia mpya na tulitumia karibu dola 5 bilioni (karibu Sh600 bilioni) mwaka jana pekee kuhusu usalama na ulinzi."

***— BBC***

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

TANZIA

■ ALICHEZA SINEMA YA KWANZA 'TOP GUN' MWAKA WA 1986

# TEXAS 'RANGER' GILYARD AAGA

## Alicheza na Chuck Norris katika 'Walker, Texas Ranger' akiwa mshirika wake 'Jimmy'



Waigizaji nyota wa sinema ya *Walker, Texas Ranger* Clarence Gilyard, Chuck Norris, Sheree J. Wilson na Noble Willingham. Gilyard alikufa Jumatano.



● NEW YORK

Clarence Gilyard, mchezaji sinema ambaye maarufu kwa nafasi aliyoshiriki katika sinema kama Walker, Texas Ranger, Die Hard na afisa wa meli kwa jina Marcus 'Sundown' Williams katika filamu inayoitwa Top Gun, ameaga dunia akiwa na umri wa miaka 66. Kifo chake kilitangazwa Jumatatu katika taarifa kutoka Chuo Kikuu cha Nevada, Las Vegas (UNLV), ambako amekuwa akifanya kazi kama profesa mwandamizi katika Kitivo cha Sanaa. "Ni kwa huzuni kuu kwamba natangaza habari hii," Mkuu wa kitivo hicho, Nancy Uscher, akasema kwenye taarifa kupitia mtandao wa kijamii wa Instagram. "Wanafunzi wake walihamasishwa naye, sawa na waliomfahamu. Alikuwa na vipawa vingi visivyo vya kawaida na alijulikana sana katika chuo kikuu kupitia kujitolea kwake kufunza na aliyoafikia katika taaluma yake."

Mwenyekiti wa UNLV Film, Heather Addison, alimkumbuka Gilyard kama "nguzo ya nuru na nguvu ya kila mtu aliyekuwa karibu naye katika UNLV". Akaongeza: "Kila tulipomuuliza habari zake, alijibu furaha kuwa alikuwa 'amebarikiwa!' Lakini kwa kweli ni sisi tuliokuwa tumebarikiwa kuwa wenzake na wanafunzi kwa miaka mingi. Tunakupenda na tutakukosa sana, Profesa G!"

Kulingana na UNLV, Gilyard alianza uigizaji baada ya kusomea Sanaa ya Uigizaji katika Chuo Kikuu cha Jimbo la California. Aliigiza mara ya kwanza katika kipindi cha televisheni 'Different Strokes' mnamo 1981. Kutoka 1993 hadi 2001, Gilyard alifana akiigiza na Chuck Norris katika 'Walker, Texas Ranger' kama mshirika wake James 'Jimmy' Trivette, nafasi ambayo alicheza tena katika 'Walker Texas Ranger 3: Deadly Reunion', 'Sons of Thunder' na 'Walker, Texas Ranger: Trial by Fire'.

Mnamo 1986, Gilyard alishiriki filamu yake ya kwanza 'Top Gun', ambayo aliigiza kama 'Sundown', mmoja wa marubani wa ndege ya kivita. Baadaye alicheza kama Theo, mtaalamu wa kompyuta anayesaidia kundi la kigaidi la Hans Gruber, katika sinema iitwayo 'Die Hard'. Alipata nafasi kubwa katika vipindi vya runinga mnamo 1989, alipocheza kama Conrad McMasters katika igizo la masuala ya sheria, 'Matlock' katika NBC, akiwa na Andy Griffith.

Gilyard pia aliigiza katika sinema kama vile 'The Karate Kid Part II', 'CHiPS' na 'Left Behind'.

Licha ya kufaulu katika fani hii, Gilyard aliacha uigizaji mnamo 2006 na kuanza kufunza katika UNLV na kuelekeza michezo katika Ukumbi wa Michezo ya Kuigiza wa Nevada Conservatory Theatre wa chuo hicho.

"Napenda kufunza. Mimi ni mtaalamu, lakini taaluma lazima ifaidi wanafunzi darasani. Hiki ndicho kinachochea wahusika wangu kwa sababu naelewa maisha ya watu karne ya 21," akaambia Jarida la Review la Las Vegas mnamo 2017. "Ninafanya vyema kama mwanasanaa nikiwa katika hali inayoruhusu. Hii inamaanisha kuwa mbunifu. Kuwa na watu hao wote wa kizazi hiki cha milenia - sielewi wanachosema lakini ninafyonza nguvu zao."

Hata hivyo, alirudi, ingawa kwa kipindi kifupi katika uigizaji mnamo 2021, alipoungana na Bruce Willis na De'voreaux White kwa tangazo la kibiashara la betri inayoitwa 'Die-Hard'. Gilyard aliigiza sehemu za wahusika katika vipindi vya runinga kama 'The Facts of Life', '227', 'Simon & Simon', na 'Riptide'.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep





**SMS the word GAZETI to 20567,**
Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE SMS text and FREE Delivery**

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

Terms & Conditions apply*



SPORT ON!
JAMES
WOKABI
BERNARD
NDONG
HOSTS
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
SATURDAYS 3PM